SportPesa
MSHINDI WA JACKPOT BONUS MECHI 12
TZS. 23,779,770
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mradi** wa uwekezaji wa Dola milioni 200 utakavyoleta ajira

UKURASA 4



**Dybala, Morata kuikosa Chelsea**

UKURASA 23

Nipashe
Jumanne Septemba 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580717
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia akerwa chanjo ya corona majumbani



• **Kuwatumbua** wakurugenzi, ma-DC, wanaogombana • **Aagiza** masoko yasiyotumika... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT) katika ukumbi wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WAZIRI JAFO ATOA SIKU 45 MAKONTENA KUTEKETEZWA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ametoa siku 45...

UKURASA WA 5

**WAHAMIAJI HARAMU 21 WATIWA MBARONI**

JESHI la Uhamiaji wilayani Kahama mkoani Shinyanga linashikilia wahamiaji haramu...

UKURASA WA 7

**UDHIBITI WAANZA UPOTEVU DAWA HOSPITALI ZA UMMA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema...

## Askofu ampa Rais kilio cha tozo miamala

UKURASA 4




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), akimkabidhi Katibu Mkuu wa ALAT, Elirehema Kaaya (kulia), mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 150 ikiwa ni udhamini wa NMB, kwa ajili ya mkutano mkuu wa jumuiya hiyo, ulioanza jana, jijini Dodoma. Wanaoshuhudia nyuma ni maofisa waandamizi wa NMB. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Shahidi aieleza korti jinsi alivyomfahamu Mbowe

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA KUANZA KUTETEA UBINGWA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Samia akerwa chanjo ya corona majumbani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wataalamu wa afya nchini, kutoa elimu kwa wananchi ili wahamasike kuchanja chanjo ya Uviko-19 badala ya kuendelea kutumia njia wanayotumia sasa ya kutembea nyumba kwa nyumba kuchanja watu.

Akifungua mkutano mkuu maalum wa uchaguzi kitaifa wa Jumuiya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), jijini Dodoma jana, Rais Samia alisema toka amerudi kutoka kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN), amekuta mtindo ambao hajauelewa wa watu kutembea na mkoba na sindano na chanjo ya nyumba kwa nyumba.

"Jamani nilisema chanjo ni hiari siyo lazima, hivyo anayetaka ndiyo achanjwe sio kulazimisha," alisema.

Alitahadharisha kuwa utaratibu huo wa kutembea nyumba kwa nyumba anahisi hautafanikiwa kutokana na namna zoezi hilo linavyoendeshwa.

"Mtaalamu unaweza kwenda katika nyumba na kumwambia mtu unataka kuchanja akasema sitaki ukaondoka, lakini kumbe kama elimu ingetolewa ya kutosha basi hili jambo lingekuwa jepesi sana."

Aliwataka wataalamu wa afya kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuwahamasisha kuchanja kwa hiari yao bila kutumia mabavu.

"Badala ya kutembea nyumba kwa nyumba basi kwanza tuandae kampeni kabambe ambayo itasaidia kufikisha elimu kwa wananchi wetu ili watambue umuhimu wa kupata chanjo ya Uviko-19 na kupunguza vifo vitokanavyo na janga hili," alisema Rais Samia.

Kadhalika, alisema hivi sasa wananchi wanaonekana kuwa wagumu kupata chanjo kutokana na kutopatiwa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo.

"Kuna mtu anaweza kuwa mgumu kupata chanjo kwasababu hajapata ile adha ambayo wengine wameipata kama kuondokewa na ndugu yake wa karibu au mjomba wake, akaona namna ambavyo ugonjwa huu ulivyo hatari njia pekee ya kuwakomboa hawa ni kuwapatia elimu ya kutosha," alisisitiza.

Aliwataka viongozi wa Mamlaka za Tawala za Mitaa nchini kuhakikisha suala la Uviko-19 wanakwenda kulishughulikia ipasavyo katika maeneo yao.

"Hili suala la Uviko-19 nataka mkalishughulikie ipasavyo katika maeneo yenu ili watu wajitokeze kupata chanjo na kuchukua tahadhari zote ambazo zinaweza kusababisha maambukizi ya virusi vya corona," alisema.

Rais Samia, alisema kutumia kampeni kuelimisha kutasaidia wananchi kujitokea kwa hiari yao kuliko kuendelea kutumia mabavu kulazimisha watu kuchanja.

Alisema vipaumbele katika awamu yake ni kuboresha sekta ya afya, elimu, maji na miundombinu.

Pia, alisema alipoingia madarakani takribani tarafa zaidi ya 200, zilikuwa hazina vituo vya afya.

"Sasa tunapeleka fedha hivi sasa ili tarafa zote hizo zipate vituo vya afya, lakini nimeambiwa hivi sasa tuana upungufu wa vyumba vya madarasa 11,000 kuna kafedha nimekapata sehemu tunakwenda kujenga madarasa 15,000 ili mwakani watoto wote waanze masomo kwa siku moja bila kuchelewa," alisema.



Meneja wa Kampuni ya Canon General Supplies inayotengeneza kinywaji cha Zhimwa ya mkoani Shinyanga Kanda ya Dar es Salaam, Sufian Mjema (kushoto), akipokea cheti cha alama ya ubora kutoka kwa Rais wa chemba ya Viwanda, Biashara na Kilimo, Paul Koyi, katika hafla iliyofanyika Makao Makuu ya Shirika la Viwango mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakuu wa wilaya, wakurugenzi wanaogombana kutumbuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza kukerwa na ugomvi kwa watumishi wa umma wakiwamo wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri na kuahidi kuwa hatozungumza kitu, bali kalamu yake ndiyo itakayozungumza.

Samia, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT).

Alisema amekuwa akishangazwa na namna ambavyo viongozi wa umma aliowateua kwenda kumwakilisha wakiacha majukumu yao na kufanya mambo yenye maslahi yao binafsi.

"Siyo kama hatuwaoni, tunawaona sana mnavyolumbana badala ya kutatua kero za wananchi, ambazo ndizo zimewaweka katika nafasi hizo mlizonazo sasa,"alisema Rais Samia.

Aidha, alisema kutokana na ugomvi huo maeneo hayo yamekosa maendeleo na kuwafanya wananchi kuendelea kupata shida ya huduma mbalimbali za jamii, ikiwamo afya, elimu na miundombinu ya barabara.

"Unakuta mambo yanakwama kutokana na maslahi ya kiongozi mmoja DC anasema hivi na DAS naye anasema vingine, lakini mkurugenzi naye anakuwa na maamuzi yake na kufanya kushindwa kuwahudumia wananchi katika kuwatatulia kero mbalimbali,"alisema Rais Samia.

Vilivile, alisema hali hiyo inatokana na viongozi kila mmoja kuwa na maslahi yake binafsi ya kutaka kutumia vibaya fedha za maendeleo zinazotumwa na serikali katika halmashauri husika.

"Huu ugomvi ni kwa sababu kila mmoja anataka kuona ni kwa namna gani atanufaika na fedha za miradi zilizotumwa na serikali katika halmashauri husika na kuzua ugomvi usiokuwa na tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla,"alisema.

Alisema hivi sasa yeye hatozungumza kitu chochote na kiongozi yeyote atakayeona anakwenda kinyume na matarajio yake au majukumu yaliyomweka katika nafasi yake.

"Kuna watu hivi sasa wananisikiliza na kusema huyu mama hakuna kitu, lakini mkumbuke mimi sijaumbwa hivyo kumkalipia mtu wala sijalelewa hivyo, lakini nawasoma tu na katika kipindi hichi cha miezi sita nimewasoma na nyinyi mmenisoma, hivyo kazi iendelee.

"Lakini nikiona hufai sina haja ya kukuita kukukaripia au kukuelekeza, nakutoa tu na nafasi yako anachukua mtu mwingine... hakuna haja ya kulea, sisi wote ni watu wazaima tunalelewa na majukumu yetu," aliongeza.

Rais Samia, alisema kutokana na Tanzania kuwa na watu wengi wenye uwezo haoni haja ya kugombana na watu aliowachagua kumwakilisha katika nafasi mbalimbali, bali atatumia kalamu kuwawajibisha ipasavyo.

"Mimi sina muda wa kumwita mtu na kuanza kumgombeza eti kwa nini hujafanya kitu fulani, wote hapa ni watu wazima na mnajua wajibu wenu, ukifanya ovyo sina muda wa kukuvumilia nakutoa naweka mtu mwingine,"alisisitiza Samia.

Kadhalika, alisema serikali inatambua umuhimu wa mamlaka za serikali za mitaa kuwa ni kiungo muhimu kati ya serikali na wananchi.

"Kwa kutambua hilo ndiyo maana Wizara ya TAMISEMI, ndiyo imekuwa ikiongoza kwa bajeti ambapo katika mwaka huu wa fedha imepangiwa kiasi cha Sh. trilioni 7.3 sawa na asilimia 20 ya bajeti yote ya serikali," alisema.

## ...Aagiza majengo masoko yasiyotumika kukodishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza majengo ya miradi ya masoko katika halmashauri mbalimbali nchini ambayo yalijengwa bila kushirikisha wananchi na kusababisha kukosa watu yakodishwe kama kumbi za harusi, ili kuiingizia mapato serikali.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa kitaifa wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT).

Alisema, moja katika ya jukumu la Tawala za Mitaa ni kuhakikisha kuwa miradi yote inayoanzishwa inashirikisha wananchi ili iwe na tija.

Rais Samia alisema kutoshirikisha wananchi katika uanzishwaji wa miradi kama hiyo ya masoko ndiko kumesababisha kukosekana kwa watu.

"Miradi yote lazima ishirikishe wananchi, pia thamani ya fedha lazima ionekane, lakini leo hii unakuta kuna majengo mazuri ya masoko ambayo yametumia kiasi kikubwa cha fedha hakuna tija kwa serikali wala wananchi kana kwamba upembuzi yakinifu haukufanyika," alisema Samia.

Aidha, alisema amekuwa akitembelea miradi kama hiyo na kuona namna ambavyo imeshindwa kuleta tija, licha ya viongozi wake kutaka kutumia nguvu nyingi kuwalazimisha watu kwenda katika masoko hayo.

"Unakuta jengo zuri na limetumia kiasi kikubwa cha fedha, lakini watu hakuna, soko la watu zaidi ya 200 walipo ni 20 na fedha nyingi zimetumika, lakini hakuna watu basi yakodisheni tu kama kumbi za harusi ili halmashauri zipate mapato,"alisisitiza Rais Samia.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa ALAT watakaochaguliwa kwenda kuhakikisha kuwa katika halmashauri matumizi ya TEHAMA yanatumika katika kukusanya mapato, kutoa huduma ikiwamo utatuzi wa migogoro ya ardhi.

"Lakini twende tukatimize malengo ya maendeleo endelevu (SDGS) kusimamia makusanyo ya mapato na matumizi ya fedha hizo za mapato.

"Juzi nilikuwa naangalia taarifa moja nikaona Waziri Mkuu anagoma kuzindua kibanda ambacho kimetumia mamilioni ya shilingi, lakini kimwonekano kibanda kile kilitakiwa kugharimu kama milioni tatu au nne tuu," alisema.

Alisema, hivi sasa serikali inapeleka kiasi kikubwa cha fedha kwenye miradi ya maendeleo, lakini mapato yanayokusanya katika halmashauri ni kidogo.

## HABARI KITAIFA

# Shahidi aieleza korti jinsi alivyomfahamu Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MSHTAKIWA wa tatu katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, Mohammed Ling'wenya amedai Luteni Denis Urio, alimtafutia kazi ya ulinzi kwa Mbowe.

Ling'wenya ambaye ni shahidi wa pili katika kesi ndogo ya madai, alidai kuwa mshtakiwa Adamu Kasekwa aliteswa kabla na wakati akitoa maelezo ya onyo.

Alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Mustapha Siyani.

Akiongozwa na Wakili John Mallya, alidai alimfahamu Mbowe mwaka 2020, baada ya kupigiwa simu na Luteni Denis Urio akimweleza kuna kazi ya kumpa ulinzi kiongozi, lakini hakutaja ni kiongozi gani.

Alidai Urio aliwahi kufanya naye kazi Kikosi 92 KJ kabla hajaachishwa mwaka 2017 na pia alimwambia yuko Mtwara ana kazi, lakini akirudi nyumbani atampa simu baba yake azungumze naye akikubali atakwenda.

Shahidi huyo alidai aliporudi alimpa simu baba yake akazungumza na Luteni Urio akakubali na kumruhusu akafanye hiyo kazi.

Pia, alidai kwenda Moshi na Kasekwa kuzungumza na mwajiri mtarajiwa ambaye alimtaja kuwa ni Mbowe, lakini kabla hawajamalizana, Agosti 5, 2020 walienda kula chakula Lau Madukani na wakakamatwa.

Ling'wenya alidai mahakamani hapo kuwa alianza kukamatwa Kasekwa akiwa pembeni anaongea na simu, kwa kuwekewa bastola na dawa za kulevya, vitu ambavyo alidai anajua mwenzake hakuwa navyo kwasababu alikuwa naye safarini.

Aliendelea kudai kuwa alipoona kawekewa vitu hivyo, alitoa simu na pochi yake ikiwa na Sh. 300,000 na kuiweka chini barazani na vyote vilichukuliwa na polisi na hajui vilipo.

Askari zaidi ya watano alidai walimpiga Kasekwa, kisha wote wakawapeleka Kituo cha Polisi Moshi ambako kwa nyakati tofauti walipigwa.

Ling'wenya alidai kila mmoja aliwekwa katika selo yake, lakini kuna wakati alimuona Kasekwa akipitishwa huku akiwa ameinamisha kichwa chini na kupelekwa katika chumba kingine kituoni hapo.

Hata hivyo, alidai hakuona ndani alikuwa anafanywa nini, lakini alisikia sauti ya kulia ikiashiria alikuwa anapigwa, alijua sauti ile aliita sauti ya zege na baada ya muda alimuona anarudishwa akiwa ameshikwa na watu watatu huku ameinamisha kichwa.

"Walikuja kunifuata mimi, nilipochukuliwa chumba kilikuwa kidogo, niliwakuta watu wanachukua video, nilihojiwa majina yangu na mahali nilipotoka, nikasema Mtwara nikapigwa buti na Inspekta Mahita Omary.

"Nilifungwa pingu mikononi na miguuni nilifungwa kamba nikaning'inizwa kichwa chini miguu juu, nilipigwa na rungu la shaba nzito katika nyayo wakitaka nisema kazi ipi iliyonipeleka Moshi.

"Nilipigwa na Mahita, alitokea askari mmoja naona ana cheo kikubwa akawaambia acheni kumpiga, aliacha kunipiga wakanipeleka mahabusu," alidai shahidi huyo.

Alipoingia mahabusu alimwita Adamu akasikia akiitika, akamuuliza vipi alimjibu yuko hoi, naye alimjibu pia yuko hoi kutokana na kipigo.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (katikati), akitoka chumba cha mahabusu ya Mahakama ya Divisheni ya Uhujumu Uchumi, kuingia mahakamani kusikiliza mashtaka yanayomkabili jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Anadai Agosti 7, 2020 alitolewa kwa ajili ya kupelekwa Dar es Salaam, akiwa kwenye gari alimwona Kasekwa akitoka anaburuzwa, akiwa kashikwa hawezi kutembea.

Alidai Mahita alirusha shuka zito wakamfunika kichwa na kulifunga hakuona kinachoendelea hadi walipofika Kituo cha Polisi Tazara.

Shahidi alidai, wakiwa njiani hawakula chakula, walipofika walishushwa lakini hakujua mwenzake yuko wapi.

Walishushwa Kituo cha Polisi Tazara, jina la mahali walipo alifahamishwa na mahabusu katika chumba cha pili, alimwambia mwenzake yupo chumba kingine.

Alidai kuwa yule mahabusu alikuwa mwanajeshi wa Kikosi cha Twalipo, alimwambia yuko mahabusu mwezi wa nane.

Mshtakiwa wa pili Adamu Kasekwa akimalizia ushahidi wake wakati akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, alidai alipofika Dar es Salaam akitokea Moshi alifikishwa Kituo cha Polisi Tazara na akiwa katika kituo hicho hakuwahi kuteswa.

Alidai kuwa alipewa ugali na mboga za majani na kupelekwa Kituo cha Polisi Mbweni ambako pia hakupigwa bali alipata vitisho kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ramadhan Kingai, ambaye anadai alimtaka asaini nyaraka alizokuwa nazo ambazo alizisaini bila kujua kiliandikwa nini.

Mshtakiwa huyo alitakiwa kueleza lipi sahihi kati ya hoja ya pingamizi kwamba aliteswa kabla na wakati anachukuliwa maelezo na majibu aliyotoa mahakamani jana kuwa akiwa Dar es Salam hakupigwa.

Mshtakiwa aliomba swali hilo lirudiwe mara kadhaa kwamba halielewi, Wakili alirudia zaidi ya mara tatu ndipo mshtakiwa alipofafanua kwamba alikuwa katika mateso sababu alifungwa pingu, lakini hakupigwa.

Wakili Chavula alitaka shahidi aeleze lipi sahihi kati ya maelezo kwamba alichukuliwa maelezo kwa mateso na aliletewa nyaraka akasaini.

Swali lilichukua muda mrefu bila kujibiwa na mshtakiwa akitaka lirudiwe. Jaji Siyani alirudia kumuuliza kwa ufafanuzi na kutaka aseme achukue jibu lipi.

Kasekwa alimwambia achukue majibu yote kwa sababu aliteswa Moshi.

Alipoulizwa alifuata nini huko, akajibu alikuwa katika kuingia makubaliano ya kazi ya ulinzi na mshtakiwa Mbowe na kwamba hayo ni maelezo na hajui aliyosaini kama ni hayo au la.

Alidai alitoa maelezo kwa mateso na alisaini maelezo bila mateso akiwa Kituo cha Polisi Mbweni.

Mshtakiwa huyo ambaye ni shahidi wa kwanza katika kesi ndogo alidai Moshi alipigwa na rungu la chuma katika magoti, kwenye nyayo, lakini hakupata vidonda isipokuwa damu ilivilia.

Wakili Chavula alidai mshtakiwa alipata tatizo la afya ya akili kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, alipelekwa Hospitali ya Lugalo kwa ajili ya matibabu na aliachishwa kazi kwa utovu wa nidhamu si kwa matatizo ya afya ya akili kama anavyodai, alitaka mshtakiwa ajibu lipi sahihi.

Kasekwa alidai hawezi kujibu lipi sahihi kati ya madai kwamba aliachishwa kazi kwa utovu wa nidhamu ama aliachishwa kazi kutokana na tatizo la akili na alikana kutumia dawa za kulevya. Mshtakiwa huyo alimaliza kutoa ushahidi.

Washtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Halfani Bwire, wote wanashtakiwa kwa mashtaka sita ikiwamo kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi kwa kulipua vituo vya mafuta na kudhuru viongozi wa serikali.


**MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD**

P.O. Box 61424 DAR ES SALAAM, TANZANIA
TELL: 0787129539/0719656930
Dealers in: Auctioneer & Debt collection
Email: mabundacompanyltd@gmail.com

**NOTISI YA SIKU 14 KULIPA DENI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa mamlaka tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** tunatoa notisi kulipa deni unalodaiwa na Benki hiyo ndani ya **siku 14** kuanzia tarehe ya tangazo hili, kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana iliyowekwa ili kufidia deni. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo, terehe na muda tajwa kama ilivyoorodheshwa hapo chini:

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | CRISTOPHER MARWA MKAMI | CT NO. 52444LR, PLOT NO. 15, BLOCK "C" NKENDE AREA TARIME | 12/10/2021 SAA 03:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14.
2. Mnunuzi akishindwa kumaliza salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
3. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyumba/kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
4. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.
5. Kiwanja/mali itauzwa mahali na kama ilivyo.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
MKURUGENZI MTENDAJI,
**MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD**
S.L.P. 61424,
DAR ES SALAAM.
**SIMU: 0624 948 058/ 0787 129 539/ 0655 129 539**
EMAIL: mabundacompanyltd@gmail.com

**AU**
**BANK OF AFRICA LTD**
HEAD OFFICE: NDC DEVELOPMENT HOUSE,
OHIO STREET/KIVUKONI FRONT,
**P.O.BOX 3054**
DAR ES SALAAM, TANZANIA.

216480402



QUEENSWAY TRUSTEES (1998) LIMITED
Cheti cha usajili namba 34463
Sheria ya makampuni, 2002
(KIFUNGU 334 (1))

MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha Queensway Trustees (1998) Limited (kampuni), yenye usajili namba 3446, kilichofanyika tarehe 18 May 2021 azimio maalumu lilipitishwa:

1. kufuatana na kifungu 331 (1) (b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. wanahisa wamemteua Joseph Lyimo wa Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

JOSEPH CYNOCK LYIMO
MFILISI wa QUEENSWAY TRUSTEES (1998) LIMITED

216479302

# Askofu ampa Rais kilio tozo miamala ya simu

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, ameiomba serikali kuendelea kuangalia tena tozo za miamala ya simu, kwani wananchi bado wanaendelea kunung'unika.

Alitoa ushauri huo mjini Babati wakati wa Jubilee ya miaka 75 ya kanisa hilo iliyofanyika Uwanja wa Kwaraa.

Askofu Konki alisema ni vizuri serikali ikawasikiliza wananchi juu ya manung'uniko waliyonayo ya tozo, kwamba wengi wao bado hawamudu gharama za makato.

"Rais Samia Suluhu Hassan namwomba awasikilize wananchi wanaumia sana juu ya tozo, siyo vizuri kuongoza watu wanaolalamika. Itafutwe namna ya kufanya," alisema Askofu Konki.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema tozo bado zinawaumiza Watanzania, hivyo ni vizuri washauri wa Rais Samia waone namna nzuri ya kumshauri juu ya suala hilo ili afanye maamuzi ambayo yatakuwa na baraka.

Aidha, alikemea tabia ya baadhi ya viongozi wa serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanaochukia watu kwa kuikosoa serikali na kuwa maadui.

Konki alisema mtu anapoikosoa serikali siyo vizuri kumchukia kwa kuwa anakuwa na nia nzuri ili serikali iweze kujirekebisha na kuboresha huduma.

Wakati huo huo, aliwashauri wananchi kuendelea kutumia njia ya maombi ili kujikinga na ugonjwa wa virusi vya corona, huku akimwagia sifa Hayati Rais John Magufuli kuwa aliacha historia ya imani na kuhamasisha Watanzania kumwomba Mungu ili kuutokomeza ugonjwa huo.

"Watanzania tuna tabia ya kujisahau, tunatakiwa kuomba ili Mungu atuepushe na corona, maombi ya kanisa ni muhimu sana," aliongeza Askofu Konki.

Aliwataka wananchi kumwombea Rais Samia ili akifanya maamuzi yawe na maslahi mapana kwa Taifa.

Kuhusu Jubilee hiyo, Askofu Konki alisema wanakumbuka jitihada za Wamisionari kutoka Uingereza na nchi nyingine za kiafrika walivyounga mkono kanisa hilo.

Alisema wamedhamiria kufufua miundombinu ya afya hasa Zahanati ya Msola iliyopo Wilaya ya Bagamoyo, ambayo ilianzishwa na Wamisionari chini ya kanisa hilo.

Alisema miundombinu sasa hivi imeimarishwa kutokana na juhudi za Wamisionari walizozifanya huko nyuma hasa barabara zilijengwa kwa kiwango mpaka sasa zinatumika.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema serikali inatambua mchango wa taasisi za dini. Aliahidi kuendelea kushirikiana na taasisi za dini na atakuwa akiwatumia kuhamasisha shughuli za maendeleo.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Dk. Emmanuel Mkony, alisema asilimia 60 ya Watanzania endapo wakichanja ugonjwa huo utakuwa umedhibitiwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (kushoto), akitoa maagizo kwa Meneja wa Mamlaka ya Mapato nchini katika Bandari ya Dar es Salaam, Florence Mniko (watatu kulia) wakati wa ziara yake ya ghafla kukagua makontena yaliyobeba mifuko ya plastiki yaliyohifadhiwa bandari kavu ya Ubungo jana. **PICHA: FAUSTINE FELICIAN**

## Waziri Jafo atoa siku 45 makontena kuteketezwa

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ametoa siku 45 kwa Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania bandarini, Florence Mniko, kuteketeza makontena matano yenye mifuko ya plastiki yaliyotelekezwa Bandari Kavu ya Ubungo, Dar es Salaam.

Alitoa maagizo hayo jana alipofanya ziara ya kushtukiza ya kukagua makontena hayo kwenye Bandari Kavu ya Ubungo, kuwataka TRA, TPA na Baraza la Taifa ya Uhifadhi na Utunzaji Mazingira (NEMC) kushiriki kuteketeza mifuko hiyo ambayo imepigwa marufuku kutumika hapa nchini. Makontena hayo yalikuwa yanasafirishwa kuelekea nchini Malawi lakini yamekaa bandarini kwa zaidi ya mwaka mmoja.

"Nawapa siku 45 kuteketeza mifuko hii chini ya usimamizi wa NEMC na baada ya hapo naomba nipate ripoti yake, hawa waliotelekeza makontena haya wana mbinu nyingi na wanazunguka sana maofisini, sasa jambo hili nimelifunga rasmi na natoa hizo siku 45 kuteketeza mifuko hii," alisema Jafo.

Meneja wa TRA Bandarini, Mniko, alisema makontena hayo yalikuwa safarini kwenda Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), yalikaa bandarini zaidi ya siku 21 zinazoruhusiwa kisheria, lakini baadaye yalitelekezwa na waagizaji wa makontena hayo," alisema Mniko.

Alisema sheria ya nchi hairuhusu matumizi ya mifuko ya plastiki, TRA haiwezi kuuza mizigo kwenye kontena hivyo sasa njia pekee ni kuyateketeza.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa NEMC, Bernad Kongola, alisema kuwa makontena hayo yapo matano na yalikuwa njiani kuelekea Malawi.

"Tulipata taarifa kuna watu walitaka kununua mizigo hii, lakini sheria yetu iliyoanza kutumika Juni 2019 inapiga marufuku uingizaji na matumizi ya mifuko ya plastiki, lakini sheria hii ipo kimya aielezei juu ya jambo kama hili la kupitisha bidhaa hizi zilizopigwa marufuku matumizi yake hapa nchini, sasa hawa wametelekeza hivyo serikali itachukua hatua ya kuteketeza," alisema.

Serikali ilipitisha sheria ya kupiga marufuku uingizaji na matumizi ya mifuko ya plastiki Juni, mwaka 2019, ili kutunza mazingira baada ya kuonekana mifuko hiyo inachafua kwa kiasi kikubwa mazingira.

## Uwekezaji wa Dola milioni 200 utakavyoleta ajira 7,000

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Israel imetangaza mipango ya kuingiza Dola milioni 200 katika sekta ya viwanda vya kilimo nchini, uwekezaji ambao unatarajiwa kuajiri zaidi ya watu 7,000.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi huo mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Smart Holding, Avi Postelnik, alisema wako kwenye mchakato wa kuandaa mazingira wezeshi ya kuanza kwa mradi huo, ambao idadi kubwa ya wafanyakazi itakuwa ni ya wazawa.

Alisema kwa sasa wapo kwenye mazungumzo na Chama cha Benki Tanzania (TBA), ili kuunda utaratibu wa kufadhili mradi huo, ambao unajumuisha kupata wafadhili washirika watakaotoa mtaji.

Postelnik alisema kampuni hiyo pamoja na mambo mengine, itamiliki shamba la ng'ombe wa nyama zaidi ya 2,500, vyakula vya ng'ombe na zingine 1,500 za maziwa yatakayokuwa yanakamuliwa kisasa.

Alisema kiwanda hicho cha ng'ombe kitahusika pia kutengeneza na kuchakata bidhaa za maziwa.

"Tutakuwa na machinjio ya kisasa ya kuchinja na kufungasha nyama, kusafisha ngozi ya ng'ombe na huduma zingine za machinjio, ambazo zitakuwa zinatolewa, pia kwa wakulima wengine wa kilimo cha ng'ombe nchini," alisema.

Postelnik alisema mradi huo utakapoanza utakuwa na machinjio ya kisasa ya usindikaji wa bidhaa za nyama ya ng'ombe na kusafisha ngozi.

Alisema huduma hizo za machinjio itatumiwa pia na wafugaji wengine wa nyama kote nchini.

Alitaja mradi mwingine utakaofanyika ni wa ufugaji wa kuku, ambao utagawanyika sehemu kadhaa ikiwamo shamba la kusambaza takriban tani 26,000 za kuku kwa mwaka.

"Mradi huu wa kuku utakuwa na shamba la kuzalisha na kusambaza kwenye soko mayai karibu milioni 60 kwa mwaka na kusambaza vifaranga.

Postelnik alitaja mradi mwingine utakaotekelezwa ni ufugaji wa samaki, ambapo kutakuwa na mashamba na mabwawa yatakayozalisha sato tani 10,000 kwa mwaka.

Alisema mashamba hayo yatajumuisha mabwawa yatakayotengwa, kwa ajili ya kuzalisha vifaranga vya samaki.

Pia alisema kutakuwa na mradi wa usindikaji wa minofu ya samaki na uzalishaji wake, ambao utalenga soko la ndani na la kimataifa.

HABARI KITAIFA

# NMB yadhamini mkutano wa ALAT kwa mil. 150/-

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB imedhamini mkutano mkuu maalum wa uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) kwa Sh. milioni 150.

Pia imejivunia makusanyo ya zaidi ya Sh. trilioni 6 kupitia Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali Kielektroniki (GePG) katika kipindi cha miaka mitatu iliyoishia Julai 2021.

Mkutano mkuu maalum wa uchaguzi, ALAT Taifa ulifunguliwa jana, kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma na Rais Samia Suluhu Hassan, aliyeambatana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Job Ndugai na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Ummy Mwalimu.



Afisa Mtendaji Mkuu wa benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema wanajivunia ushirikiano wao na ALAT, ambao umekuwa chachu ya kudhamini mara kwa mara mikutano yao hiyo na kuwa anaamini jumuiya hiyo itauenzi uhusiano huo, huku wakiendelea kuifanya NMB kuwa benki namba moja katika makusanyo ya halmashauri zote nchini.

"Matarajio yetu ni kuendekeza uhusiano mwema kati ya ALAT na NMB na ushirikiano mzuri na halmashauri zote katika kukamilisha miradi mikubwa inayosimamiwa na halmashauri zetu, pia tumekuwa vinara wa makusanyo ya fedha za Serikali.

"Katika mwaka mmoja wa fedha uliopita (Julai 2020 hadi Julai 2021), NMB ilikusanya Sh. bilioni 343.9, wakati kwa miaka mitatu tumekusanya takribani Sh. trilioni 6, huku tukiwa sehemu ya ufanikishaji wa miradi na uendelezaji wa mazao ya kimkakati kote nchini," alisema Zaipuna.

Akifungua mkutano huo, Rais Samia (pichani) aliipongeza NMB kwa kubeba dhamana kufanikisha uchaguzi wa ALAT Taifa, huku akiwataka wajumbe kuchagua viongozi sahihi, ili kuitendea haki kaulimbiu ya mkutano huo isemayo 'Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu,' kwani ALAT imara ndio msingi mkuu wa maendeleo endelevu yanayochakatwa na serikali yake.

# Wahamiaji haramu 21 watiwa mbaroni

Na Neema Sawaka, KAHAMA

JESHI la Uhamiaji wilayani Kahama mkoani Shinyanga linawashikilia wahamiaji haramu 21, kutoka nchi za Burundi na Msumbiji kwa kosa la kuingia nchini, bila kuwa na vibali na kufanya kazi.

Wahamiaji hao wamekamatwa katika operesheni maalumu ya kuwasaka watu wanaongia nchini, bila ya kuwa na vibali na wengine wakifanya kazi mbalimbali za kuajiriwa kinyume cha sheria za nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Kahama, Salumu Rashid Salumu, alisema operesheni hiyo ni ya kawaida, lengo likiwa ni kudhibiti watu kutoka Nchi ya Burundi, ambao hukimbia kwao kutokana na ugumu wa maisha.

Salumu alisema wahamiaji hao wanaingia katika Wilaya ya Kahama na kufanya kazi mbalimbali, ikiwamo shughuli za kilimo cha tumbaku, kuuza mayai, karanga, kuendesha baiskeli, kuuza vitumbua, kusukuma matoroli pamoja na kazi zingine.


Alisema kundi lingine limekuwa likifanya kazi za kuchunga mbuzi, ng'ombe na kuongeza kuwa watu hao wamekuwa wakiingia nchini kwa kutumia njia za panya na wanapowafanyiwa mahojiano husema kuwa wameamua kukimbia nchini kwao, kutokana na hali ngumu ya maisha.

Aidha, Ofisa huyo alitoa onyo kwa wenyeji wanaowahifadhi wahamiaji hao kuwa ni kosa na wakikamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria kwa kuwa kwa sasa sheria zimebadilika zimekuwa kali kwa watu kama hao.

Alisema wanapowakamata wanaowahifadhi na kuwafikisha mahakamani wengi wao husema kuwa wanadanganywa na watu na kujikuta wakiwachukua, kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali.

Alisema kwa mwezi wanakamata zaidi ya wahamiaji 50 katika maeneo mbalimbali yakiwamo yale ya vituo vya mabasi na kuongeza kuwa wanapohojiwa huwa wagumu kukiri kuwa wao ni raia kutoka Burundi.

Alisema kuwa ni bora wahamiaji hao wanapokuwa wakiingia nchini wafuate taratibu husika kwa kuwa wanapokamatwa na kufikishwa mahakamani hutozwa faini Sh. 500,000 au kifungo cha miaka mitatu gerezani ama vyote kwa pamoja kwa mujubu wa sheria.w






Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utashi kisiasa muhimu TANESCO kujiendesha

**IMEBAINIKA** kuwa miongoni mwa sababu zilizokuwa zinalikwamisha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kujiendesha, mojawapo ni serikali kuingilia uendeshaji, lakini na maamuzi ya kisiasa.

Sababu hiyo na nyingine kadhaa, ndizo zinazodaiwa kulalamikiwa na wananchi mbalimbali kutokana na kutoa huduma duni, ambazo hazilingani na mahitaji ya wateja.

Hata hivyo, Waziri wa Nishati January Makamba, anaahidi kuwa chini ya uongozi mpya wa shirika hilo ulioteuliwa hivi karibuni, hakutakuwa na maamuzi ya kisiasa au misukumo ya kisiasa katika uendeshaji wa shirika hilo.

Kwa kauli hiyo, tunaona kwamba sasa serikali imedhamiria kwa dhati kufufua shirika hilo ili litoe huduma kikamilifu, hivyo tunaamini kwamba kuwapo kwa utashi wa kisiasa kunaweza kusaidia shirika kusimama imara.

Sisi tunaamini kwamba kuwapo kwa utashi wa kisiasa kunaweza kusaidia shirika hilo kufanya kazi likiwa huru badala ya kuingiliwa na baadhi ya watu kwa maslahi yao binafsi na kujikuta likishindwa kujiendesha inavyotakiwa. Wanasiasa wanapoingilia shirika wanaweza kulisababisha hasara na kulifanya lishindwe kutoa huduma inayotakiwa, hivyo kuwafanya wateja na wananchi kwa ujumla kuliona kama halina umuhimu kwao.

Kila mara tumekuwa tukisikia kwenye vyombo vya habari malalamiko ya baadhi ya wananchi kuhusu huduma duni za shirika hilo na hata lugha mbovu kutoka kwa baadhi ya wafanyakazi dhidi ya wateja wao.

Kadhalika, kumekuwapo malalamiko ya wananchi dhidi ya wafanyakazi kadhaa wa shirika ya kuwadai rushwa ili wapatiwe huduma hususan za kufungiwa umeme.

Hivyo kwa kauli hiyo ya Waziri Makamba kukiri kuwapo kwa upungufu na kuahidi kuyafanyia kazi, tunaona ni nafasi nzuri sasa kuchana shirika hilo lijiendeshe na kutoa huduma inavyotakiwa bila kuingiliwa na wanasiasa.

Tunaichukulia kauli hiyo kuwa huenda ikaleta mabadiliko makubwa kwenye utendaji kuanzia bodi, uongozi na hata mfanyakazi mmoja mmoja ili Watanzania waweze kuhudumiwa bila kikwazo.

Kumekuwapo na mkakati wa kutaka kuzalisha umeme mwingi wa kuuza nje ya nchi kwa megawati 2,100 kupitia mradi wa bwawa la Nyerere, hivyo ushauri wetu ni kwamba utashi wa kisiasa uachwe uchukue nafasi yake ili kufanikisha mikakati yote ya kuwa na nishati ya kutosha.

Tunaamini kwamba utekelezaji wa mradi huo unaotarajiwa kugharimu fedha nyingi za wananchi takribani Sh. trilioni 7 usijaribu kuingiliwa na wanasiasa kwa maslahi yao, ili nchi ijitosheleze kwa nishati ya umeme pamoja na kuuza ziara nje ya nchi. Kuwapo kwa maamuzi ya kisiasa katika uendeshaji wa shirika kunaweza kuwa na athari mbaya kwa kuwa taratibu za uendeshaji hazitafuatwa, badala yake malengo ya wanasiasa ndiyo yatazingatiwa.

Ikumbukwe kwamba maamuzi mabaya yakiwamo ya kisiasa ndiyo yaliyoifikisha TANESCO hapa ilipo ikiwamo mikataba mibovu, ambayo imeisababishia nchi hasara kubwa.

Kimsingi hilo likizingatiwa na kila upande ukatimiza wajibu, nchi inaweza kuwa na umeme wa kutosha hata kuuza nje ya nchi, na pia malalamiko kutoka kwa wateja yatapungua kutokana na huduma bora.

Kwa kuwa waziri anataka shirika hilo kibiashara, nasi tunashauri uwapo wa utashi wa kisiasa ili lengo hilo liweze kutimia, kwani huduma zinaweza kuboreshwa na kuondoa malalamiko yasiyo ya lazima kutoka kwa wateja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wabunifu, wagunduzi njia nyeupe kuachana kuajiriwa

Na Sabato Kasika

**ELIMU** ndiyo benki ya maarifa inayoondoa ujinga, umaskini na maradhi na kuotesha mawazo mapya ndani ya watu kwa kuwawezesha kutumia uwezo na rasilimali fedha, ardhi na uongozi bora, kubadilisha maisha yao na kujiletea maendeleo.

Kwa kuwa na elimu bora taifa linaongeza tija na ufanisi katika kazi, hasa elimu inayowapa ujuzi na stadi zinazolingana na uwezo na uhitaji unaotakiwa kwenye fani.

Kwa mfano, elimu ya ufundi, inatajwa kuwa ni muhimu kwa kuwajenga vijana kiuwezo, kiubunifu na kiugunduzi pia na huo ndiyo mwisho wa kuachana na mawazo ya kuajiriwa.

Inawaimarisha na kuwapa ustadi na inaweza kuwasaidia kupata ajira haraka kama stadi hizo zimejikita kwenye matarajio ya waajiri hasa kulingana na wakati.

Kwa kutambua umuhimu huo, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), imekuwa ikiwajengea uwezo wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vijana mbalimbali, ili kuwaandaa watakapohitimu masomo yao wajiajiri au waajiriwe kutokana na ujuzi unaowaongezea ubunifu.

Taasisi hiyo inawajengea uwezo wanafunzi wake kuanzia kwenye nadharia na vitendo, hali ambayo inaelezwa na Mratibu wa Mafunzo, Daud Mboma kuwa yanamfanya mwanafunzi ahitimu akiwa 'ameiva'.

Ninaamini elimu hiyo itawezesha wanafunzi kuondokana na mawazo ya kuajiriwa na badala yake wafikirie kujiajiri ili kuepusha kuzunguka ofisi mbalimbali kusaka ajira.

Uamuzi huo wa kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya soko la ajira, ni kama ule wa elimu ya kujitegemea ilijikita katika kuwajenga vijana kujifunza zaidi kazi za uzalishaji shuleni na kuziwezesha kujitegemea kutokana na uzalishaji huo.

Mbali na hizo shule kujitegemea, kazi hizo ziliwawezesha wanafunzi kujengwa kwa namna ambayo iliwapevusha fikra zao na hivyo kuleta mtizamo chanya na mabadiliko ya kweli katika jamii kutokana na ujuzi walioupata.

Wanafunzi pia mbali ya elimu ya darasani, walipewa elimu ya stadi za maisha na dhana elimu ya kujitegemea iliondoa upungufu mwingi uliokuwapo kwenye elimu ya mkoloni ambayo iliegemea zaidi kusaka watumishi wa kuitumikia.

Mpango huo wa elimu ya kujitegemea uliwafanya wanafunzi wafanane na maisha ya Kitanzania na watambue wajibu wao kwa jamii baada ya kumaliza shule na vyuo vikuu.

Nimetoa mfano huo kutokana na kile kinachofanywa na DIT, kwani kinaelekea kuhakikisha wanafunzi wanahitimu wakiwa na mawazo ya kujitegemea badala ya kusubiri ajira.

Ingawa baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakionekana kama hawapendi kilimo, ufugaji na ufundi, huku sababu kubwa ikiwa ni kwamba hayo hawafundishwi shuleni, ni vyema sasa wakaanza kuyasoma.

Wawe wamezaliwa mijini au vijijini, si vibaya wakafundishwa kilimo bora na ufugaji wa kisasa ili baadaye waweze kunufaika na shughuli.

Kila shule inaweza kuwa na mbinu za kuwaandaa wanafunzi wake kulingana na kiwango cha elimu kama ambavyo DIT inawaandaa kwa kuwafundisha matumizi ya TEHAMA ili waingie katika soko la ajira na kujiajiri.

Hivyo, ili mwanafunzi akihitimu shule aweze kujitegemea, ni vyema katika mipango ya elimu shule za sekondari zikafundisha masomo yanayofundishwa na vyuo vya ufundi (VETA).

Lakini masomo yatakayoingizwa kwenye mitaala yahusiane na mazingira yanayowazunguka, hasa kilimo, ufugaji wa mifugo na samaki, upishi, utalii na ufundi ukiwamo urejelezaji wa bidhaa.

Vilevile wanafunzi wanaweza kufundishwa, utengenezaji vitu mbalimbali vinavyotokana na bidhaa zinazozalisha nchini, na hivyo kuwafanya waweze kuendesha maisha yao bila kutegemea kuajiriwa.

Kuwapo kwa shule za aina hiyo kunaweza kusaidia kuwajenga vijana misingi ya kujitegemea na kujiamini.

## HABARI KITAIFA

## ‘Tumieni nyumba za ibada kutoa elimu chanjo ya corona’

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, amewaomba viongozi wa dini kutumia nyumba za ibada kutoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19, ili wananchi wengi wachanje, kujikinga na ugonjwa huo.

Sara aliyasema hayo jana, wakati akifungua kikao cha afya ya msingi kilichofanyika katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Alisema viongozi wa ngazi mbalimbali waliopata elimu ya UVIKO-19 wanatakiwa kuifikisha kwa wananchi na kwa viongozi wa dini wanatakiwa kuwaelimisha waumini wanaofika kwenye ibada.

“Viongozi wa dini wamekuwa wakiisaidia serikali katika vitu mbalimbali, ikiwamo kuiombea nchi kwakuwa wananchi wengi wanafika kwenye nyumba za ibada ni vyema wakaelezwa ukweli kuhusu chanjo hii na mwenye hiari aweze kuchanjwa,” alisema.

Aidha, alisema wilaya hiyo imejipanga kuwafikia wananchi wote watakao kuwa tayari kuchanjwa popote walipo.

Mratibu wa chanjo Wilaya ya Kibaha, Hadija Tellack, alisema wilaya hiyo ilipokea chanjo 7,000 na hadi sasa wataalamu wa afya wanaendelea kuchanja wananchi katika vituo 46 vinavyotoa huduma hiyo.

Kwa upande wa mkoa zilipokelewa chanjo 30,000 na hadi sasa 15,000 zimetumika na inaelezwa kuwa umesalia mwezi mmoja wa matumizi ya chanjo hizo kabla ya kuharibika.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani alieleza hivi karibuni kuwa wapo wataalamu 554 wamepata mafunzo ya kutoa chanzo na watawafikia wananchi ngazi zote hadi majumbani kwa wenye hiari ya kuchanja watafikiwa.

# Udhibiti waanza upotevu dawa hospitali za umma

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema uhaba wa dawa katika hospitali za umma nchini, unatokana na upotevu wa dawa unaofanywa na watumishi wasiyo waadilifu.

Amesema ili kudhibiti hali hiyo, serikali imeanzisha mfumo mpya wa kukusanya taarifa zote katika kila idara kwa lengo la kuongeza kasi ya uwajibikaji kwa watumishi wa wizara hiyo.

Waziri Dorothy aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kikao cha wataalamu na wadau wa masuala ya ugavi wa dawa nchini na kuwataka kuweka mpango mkakati wa kutunza taarifa ili kufahamu dawa zinapopotelea.

“Suala la upotevu wa dawa linafanywa na watu wachache ambao kwa mbinu zao wanaweza kuleta uharibifu mkubwa sana, tumebaini pamoja na serikali kuongeza bajeti ya dawa, pamoja na kuagiza dawa moja kwa moja kutoka viwandani tushushe bei pamoja na kusambaza dawa zifike kwenye vituo, kama hatujaziba kule zinapotumika zitumike vizuri tutapata uharibifu na kutokutesheleza kwa mahitaji haya,” alisema Dk. Dorothy.

Alisema suala hilo siyo usimamizi mbovu bali uwajibikaji na ufuatiliaji wa rasilimali za umma unaofanywa na watendaji wasiyo waadilifu.

“Unaweza usiwe mdokozi, lakini unanunua dawa nje ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kule gharama ni kubwa na mtaji ukaisha, lakini ukanunua MSD lakini dawa zisifike kituoni na zikafika kituoni zisifike kwa mlaji ambaye ni mgonjwa na ndio maana hizi takwimu tukiziangalia hatuzioni kwenye taarifa zetu,” alisema Dk. Dorothy.

Alisema matokeo ya mfumo wa ufuatiliaji wameanza kuyaona, ukilinganisha na miezi mitano iliyopita kabla ya kuwapo kulikuwa na upotevu mkubwa wa dawa.

“Waliofanya ufuatiliaji na waliyoyakuta kule ni makubwa, hakuna upotevu wa dawa na hakuna bajeti iliyoongezwa, tutakuja kuwaeleza kuhusiana na hili ila mfumo huu umesaidia kudhibiti upotevu kwa asilimia kubwa,” alisema.

Akizungumzia maeneo 16 ya mfumo wa ugavi wa bidhaa za afya yaliyofanyiwa ufuatiliaji katika hospitali za rufani za mikoa na thamani ya upotevu wa fedha kwa kila eneo ambao taarifa zake zilitolewa Machi 3, mwaka huu alisema ulifanyika kwa miezi 18 na idadi ya bidhaa 25-20.

Alisema walibaini ankara ambazo hazikuonekana kwenye hospitali za rufani za mikoa ni Sh. bilioni 11 na bidhaa zilizo na ushahidi wa kuwa zimetoka bohari kwenda kutumika ni za Sh. bilioni 3.2

Waziri huyo alitaja pia walibaini bidhaa zilizopelekwa kituo kingine hazijawahi kufika ni za Sh. milioni 354.7, bidhaa zilizofika kwenye idara au kitengo kutofika kwa wagonjwa Sh. bilioni 2.4 na bidhaa ambazo zilinunuliwa kwa washirika bila kibali cha MSD Sh. bilioni 5.6.

Nyingine ni bidhaa zilizonunuliwa MSD na washitiri teule Sh. bilioni 1.12, bidhaa zilizonunuliwa kwa washitiri kinyume na mkataba Sh. milioni 640, bidhaa zilizonunuliwa bila kuidhinishwa na kamati ya Dawa na Tiba Sh. Bilioni 1.9 na bidhaa ambazo wateja wanachama wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) walikosa Sh. bilioni 6.1

Naye Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi, alisema nchini kuna viwanda 18 vilivyopo katika hatua mbalimbali, vingine vimeanza uzalishaji kwa lengo la kupunguza uagizaji wa dawa kutoka nje ya nchi kutoka asilimia 88 ya sasa hadi kufika chini ya asilimia 50 mwaka 2030.

# Mhagama afurahishwa kampuni kujali maslahi ya wafanyakazi

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Ajira na Kazi, Jenista Mhagama, amewataka vijana kutokubweteka mahala pa kazi, waongeze ubunifu kusaidia kuongeza kipato na kuwa chachu ya kukua kwa uchumi wa nchi.

Mhagama aliyasema hayo juzi, jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla fupi ya utiaji saini mkataba wa hiari wa hali bora baina ya menejimenti na Kampuni za Oryx na Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO).

“Muda mwingine hata vikao vya maridhiano yanayolenga kuweka mazingira mazuri ya kazi baina ya wafanyakazi na taasisi zao, yamekuwa yakiishia njiani, lakini Kampuni ya Oryx imeliweza hilo kwa hiyo niseme tu mkataba wa hali bora kazini uliotiwa saini leo, utaleta matokeo chanya kwa wafanyakazi na kampuni yenyewe, lakini kuongeza kipato na tija ya ufanyaji kazi kwa ufanisi baina ya wafanyakazi na taasisi.”

“Mimi nafarijika sana ninapoona waajiri wanawajali wafanyakazi wao kwa kuchukua hatua stahiki kama hii ya leo, hiki ni kielelezo tosha kabisa kwamba kampuni ya Oryx, ina nia njema na wafanyakazi wake na hili ni jambo la kupongeza.”

Katika hatua nyingine aligusia baadhi ya vipengele vilivyopo katika mkataba huo na kusifu kuwekwa kwa maslahi ya mfanyakazi mbele.

Alitaja baadhi ya vipengele vilivyomfurahisha kuwa ni kuongeza muda wa likizo kwa mwanamke anapokuwa katika kipindi cha uzazi na kuzishauri kampuni zingine kutenga maeneo ya kunyonyeshea watoto katika maeneo ya kazi na kuwawekea huduma ya lishe.

Vilevile, alipongeza kipengele cha kuwalipia ada watoto wa wafanyakazi na kusema ni jambo zuri na lina leta raha.

“Nyongeza ya malipo kwa watumishi waliofanya kazi kwa muda mrefu katika Kampuni ya Oryx, mambo haya yataleta tija kubwa kwa wafanyakazi na mabosi wa kampuni na ukizingatia tunaye rais mchapakazi na mwenye maono na Amiri Jeshi Mkuu,” alisema.

Kwa upande wake Katibu Mkuu TUICO, Boniface Mkakatisi, aliwataka vijana wasibweteke na wawe na ari ya kufanya kazi kwa moyo mmoja kuongeza tija na ufanisi zaidi katika utendaji wao wa kazi.

Vilevile Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Oil, Kalpeshi Metha, alimpongeza Rais Samia, kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kuahidi kuwekeza zaidi, ili kuongeza fursa ya vijana wengi kupata ajira.




CAPITAL
TELEVISION

Kipindi kinachoangazia mabadiliko ya tabia nchi, Chimbuko, Madhara na njia mbalimbali za kujinasua na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi na kuifanya dunia kuwa sehemu salama ya kuishi.

**USIKOSE KUFUATILIA KIPINDI HIKI KITACHOANZA SIKU YA JUMANNE TAREHE 05 OKTOBA 2021 SAA 1:30 USIKU**

# CoRI yalalamika utekelezaji hafifu Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa

**Na Romana Mallya**

UMOJA wa Asasi zinazotetea Haki ya Kupata Taarifa (CoRI), umesema kumekuwa na utekelezaji hafifu na usioridhisha wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa iliyotungwa miaka mitano iliyopita na kutaka izingatiwe.

Mwenyekiti wa CoRI, Kajubi Mukajanga, akisoma tamko hilo la pamoja la Umoja huo jana jijini Dar es Salaam kuelekea siku ya haki ya kupata taarifa inayoadhimishwa leo, alisema CoRI imeona sheria hiyo ambayo sasa ina nusu mwongo tangu kupitishwa na Bunge na kupata idhini ya Rais, utekelezaji wake siyo wa kuridhisha.

Mukajanga alisema kutokana na hali hiyo, CoRI inataka kuteuliwa kwa maofisa watoa taarifa katika kila taasisi za umma wenye mamlaka na wajibu huyo wa kuzitoa zikiwamo zinazoombwa na wananchi moja kwa moja kama inavyotamkwa na kifungu cha saba cha sheria.

"Tunataka kuwapo na utoaji wa mara kwa mara wa taarifa muhimu kwa umma katika kila ofisi ya umma ikiwamo muundo wa kitaasisi, aina ya taarifa zinazopatikana katika taasisi husika na namna ya upatikanaji wake kama ilivyoelezwa katika kifungu cha tisa cha sheria," alisema.

Mwenyekiti huyo alitaja jambo la tatu kuwa CoRI inataka kuanzishwa kwa mfumo wa ufuatiliaji kubaini maombi yote ya taarifa na majibu yake kutoka ofisi za umma.

Alisema siku ya kimataifa ya haki ya kupata taarifa, inatoa fursa ya kukumbushana umuhimu wa mjadala wa kitaifa wa namna ya kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa Tanzania.

"CoRI tunaamini kuwa ipo haja ya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016; kuongeza kasi ya utekelezaji wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, 2016 pamoja na marekebisho na utekelezaji wa kanuni za sheria hizo kama njia ya kuimarisha mfumo wa kitaasisi utakaosaidia kufikia uhuru kamili wa habari.

"Pia haki ya kupata taarifa kwa kila mtu na kufikia malengo ya maendeleo endelevu kwa haraka zaidi."

Mjumbe wa CoRI, Anastazia Rugaba, alisema baada ya kuona matatizo ya upatikanaji wa habari umoja huo kwa kuongozwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), wametengeneza mwongozo wa haki ya upatikanaji wa taarifa kwa maofisa habari ambao sehemu yake itawasilishwa leo.

Alisema utakapokamilika utapatikana kwenye mitandao na itawasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ambao ndiyo wasimamizi wa maofisa habari katika maeneo yao.

Mjumbe Deodatus Balile ambaye ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuihamisha Idara ya Habari kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwenda kuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

"Tunamshukuru Rais kwa kumaliza mkanganyiko huu, maana yake tunapozungumzia masuala ya mawasiliano yanayochangia miundombinu ya habari tutakuwa na mtu mmoja," alisema.

Balile alisema mkanganyiko huo haukuishia kwa waandishi wa habari, hata maofisa habari katika nafasi zao wamekuwa hawana mamlaka kamili.

"Mamlaka yao yanatekwa na makatibu wakuu kwenye wizara au halmashauri," alisema.

Taasisi zinazounda CoRI ni pamoja na MCT, LHRC, TEF, TWAWEZA, THRDC, SIKIKA, TLS, Misa-Tan, Policy Forum, Jamii Forum, TAMWA na TCIB.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akiwasalimia machifu wa makabila mbalimbali ya nchini Ivory Coast katika mkutano wa Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani jijini Abidan, nchini jana. **PICHA: HAPPY SHAYO**

# NIT, TRES wakubaliana ujenzi wa majengo mafunzo ya anga

**Na Elizabeth Zaya**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji(NIT), kimetia saini makubaliano na Kampuni ya TRES Consult kwa ajili ya tathmini ya mazingira kwenye jamii kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya mafunzo ya anga.

Majengo hayo yanatarajiwa kujengwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere (JNIA) pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA).

Akizungumza kwenye hafla ya utiaji saini ya ujenzi wa majengo hayo uliofanyika Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo cha NIT, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema wanaamini waliopewa kazi hiyo wataifanya vizuri pasipo kuathiri mazingira kwenye jamii.

Alisema lengo la mradi huo ni kuongeza fursa pamoja na kuboresha ubora wa programu za Mafunzo ya Ufundi (VETA) katika vyuo vilivyochaguliwa ikiwamo Chuo cha NIT.

"Miradi hii inafadhiliwa na mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia chini ya mradi wa mabadiliko ya ujuzi na ujumuishaji wa Kikanda wa Afrika Mashariki (EASTRIP),"alisema Profesa Mganilwa.

Naibu Mkuu wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Chuo cha NIT, Dk. Prosper Mgaya, alisema wanaamini kwamba ujenzi wa mradi huo utakamilika kwa muda uliopangwa.

Meneja wa Kituo cha Umahili cha Mafunzo ya Anga na Usafirishaji (CoEATO) katika chuo hicho cha NIT, Abubakar Noor, alisema majengo hayo yatatumika kutoa mafunzo kwa wanafunzi ambao kwa sasa wanafanya kozi za uhandisi wa ndege ili kuongeza idadi ya wataalamu katika eneo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TRES Consult, Bashiru Abdul, alisema wamejipanga kufanya kazi kwa bidii kulingana na matakwa ya makubaliano waliyosaini.

Alisema kampuni hiyo ndiyo ilihusika katika kufanya tathmini ya mazingira katika mradi wa ujenzi wa jengo la tatu la abiria JNIA mwaka 2018.

"Kuanzia mwaka 2014 hadi 2018 kampuni yetu ilihusika katika kuangalia mazingira kwenye maeneo mengi ikiwamo ufuatiliaji wa ubora wa maji, kelele, hewa na mitetemo JNIA," alisema Abdul.

"Pia ilihusika katika tathmini ya athari za mazingira kwa mradi wa ukarabati na uendelezaji wa KIA chini ya msaada wa Orio kutoka Serikali ya Uholanzi."

# RC ataka wakulima kuepushwa lumbesa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, ameutaka Wakala wa Vipimo (WMA), kuendelea kuelimisha wakulima matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji kwani madalali wamekuwa na tabia ya kuwanyonya wakulima kwa kutumia vipimo batili kama ndoo na lumbesa.

Rubirya amesema elimu ya vipimo itasaidia wakulima kuuza mazao ya kwa kutumia vipimo sahihi vilivyohakikiwa ili mkulima aweze kunufaika kwa kupata fedha inayolingana na thamani ya mazao yake na kutaka vianzishwe vituo maalum kwa ajili ya kuuzia mazao na viewe na mizani iliyohakikiwa.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua semina ya kuhamasisha matumizi sahihi ya vipimo kwa wafanyabiashara na wakulima wa mkoa huo.

Pia ameitaka WWA kwa kushirikiana na taasisi zingine kukaa pamoja na kuhakikisha wanatoka na vifungashio ambavyo vinakubalika kwa nchi nzima hii itasaidia mazao yatakapofika sokoni yote kuwa na thamani sawa na ushindani utakao fanana kwenye soko.

Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Njombe, ambaye ofisi yake imeshirikiana na WMA kutoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya vipimo na ufungashaji kwa wakulima, alisema, mpaka sasa elimu ya vipimo imetolewa katika wilaya za Njombe Mjini, Wanging'ombe na Makete.

Alisema jumla ya wajasiriamali na wafanyabiashara 400 wamenufaika kwa kupata elimu kuhusu vipimo sahihi na namna ya kutambua kipimo kilichohakikiwa.

Pindi Chana alisema elimu hiyo imekuja kipindi sahihi kwani suala la vipimo limekuwa changamoto hasa katika Mkoa wa Njombe ambapo wananchi wanajihusisha na kilimo cha mahindi, maharage, parachichi na viazi mkulima analima kwa tabu kwa kutumia gharama kubwa, lakini wanapokuja madalali kununua mazao wanalazimisha kununua kwa vipimo batili vya lumbesa na visado.

Meneja wa WMA Mkoa wa Njombe, Hennry Msambila, alisema WMA hufanya uhakiki wa vipimo mbalimbali katika Mkoa wa Njombe na baada ya ukaguzi mkuu hufanya kaguzi za kushtukiza katika maeneo mbalimbali ili kujiridhisha kama vipimo hivyo vinatumika kwa usahihi kama vilivyohakikiwa awali.

# Wadau wa korosho wahoji fedha za makato

**Na Yasmine Protace,**

MKURANGA

WADAU wa korosho Mkoa wa Pwani, wametoa malalamiko yao kwa Mkuu wa Mkoa huo, Abubakar Kunenge, kuwa vyama vya msingi vinawakata fedha za korosho, lakini hadi sasa hawajui ni kiasi gani kilichokusanywa katika makato hayo.

Wadau hao walisema kuwa kila mkulima anakatwa shilingi mbili katika kilo moja ya korosho na fedha zinazopatikana hutumika katika mkutano wa wadau wa korosho.

Hayo yalisemwa na Diwani wa Kata ya Mbezi, kRashid Mohamed Serungi, katika mkutano wa wadau wa korosho Mkoa wa Pwani.

"Wakukima wa korosho Mkoa wa Pwani kila tunapopeleka korosho katika vyama vya msingi kuuza, huwa tunakatwa kila kilo moja ya korosho inachukuliwa shilingi mbili ambayo ndio inakusanywa kwa ajili ya kufanya mikutano wa wadau wa korosho," alisema.

Aliongeza kuwa pamoja na kukatwa fedha hizo, hawajawahi kuambiwa kiasi walichokipata katika makato hayo, ikiwamo na kuambiwa ididi ya korosho walizopokea kutoka kwa wakulima wa Mkoa huo.

Kwa upande wake, Kunenge alisema kuwa wote wanaohujumu korosho, mtandao wao wataufuatilia na kuuvunja.

"TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) naomba mshirikiane na polisi kuukamata mtandao wote unaojihusisha ya kuhujumu zao hilo," alisema.

Pia Kunenge aliwataka wakulima wa korosho kuyaboresha mashamba yao ili nao waweze kunufaika na kilimo hicho.

Kadhalika, alielekeza wakulima wote wa Mkoa huo wanaolima korosho wapatiwe msaada wa bima za mazao yao.



Sheikh wa Mkoa wa Kagera, Haruna Kichwabuta (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu sherehe za Maulid ambazo zitafanyika mkoani humo mwezi ujao. Wengine ni Mwanasheria Mwesigwa Zaidi Siraji (kushoto) na Mratibu wa Maulid Taif, Abdulrafiq Jaafar. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Taasisi yasaidia vifaa tiba watoto njiti

**Na Gwamaka Alipipi**

TAASISI ya Doris Mollel Foundation imekabidhi msaada wa vifaa tiba mbalimbali katika Hospitali ya Wilaya Maswa mkoani Simiyu, kwa ajili ya kuwahudumia na kuwalea watoto wanaozaliwa kabla ya wakati 'njiti'.

Msaada huo ni hatua katika kusaidia kupunguza safari za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kupelekwa Hospitali ya Kanda ya Rufani Bugando mkoani Mwanza kwa ajili ya kuhifadhiwa na kupewa huduma.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Doris Mollel alisema: "Nashukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwahangaikia watoto waliozaliwa kabla ya wakati na kuwa kama watu wengine. Najua kazi hii ni ya Wizara ya Afya, lakini sisi kama wadau tunafanya kazi hii kupitia miongozo yao."

Alisema msaada huo una thamani ya zaidi Sh. milioni 50, na kwamba ameshirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwamo Benki ya NCBA ambao wamekuwa bega kwa bega katika jitahada za wakusaidia watoto njiti.

Miongoni mwa vifaa tiba vilivyotolewa ni mashine mbili za kupumulia, mashine za kusaga nafaka ili kuleta ahueni kwa kinamama wanaohudumia watoto katika hospitali, magodoro, runinga, vitanda na mashuka.

Meneja wa Benki ya NCBA tawi la Mwanza, Dorin Lushiba, ambao nao wamechangia msaada huo alisema msaada huo utasaidia kupunguza hali ya kuwasafirisha watoto kwa njiti kutoka Maswa hadi Bugando kwa ajili ya matibabu kwa kuwa watakuwa na vifaa vyao kuwalea watoto hao.

"Na sisi tumeguswa kutoa msaada katika wodi ya kinamama wanaojifungua watoto njiti. Tumekuwa tukisaidia sekta ya afya, kwa sasa kunaungana na Taasisi ya Doris Mollel katika kusaidia msada huo," alisema Lushiba.

Alisema awali vifaa hivyo vilipatikana Hospitali ya Kanda ya Rufani Bugando, kwa sasa vitapatikana wilayani Maswa na kusaidia mkoa wote wa Simiyu.

Mbunge wa Maswa Mashariki, Stanslaus Nyongo, alisema: "Tunakwenda kupata vitanda vya kisasa kwa ajili ya kuwatunza watoto njiti. Oksijeni machine tatu zenye njia mbili, mizani tatu hatutakuwa na haja tena ya kuwatuma kwenye Hospitali ya Bugando.

## SMZ: Tumejipanga kwa uchumi wa bluu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imesema imejipanga kikamilifu kuhakikisha inafanikiwa katika dhana ya uchumi wa bluu katika kuhamasisha matumizi zaidi na endelevu ya bahari kwa ajili ya upatikanaji wa ajira za kudumu.

Akizungumza katika mkutano wa wadau kuhusu mapitio ya rasimu ya uchumi wa bluu uliofanyika Chakechake, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Massoud, alisema, maamuzi hayo ya uwekezaji wa uchumi wa bahari yamefikiwa kwa kutambua uwezo na mpango wa maliasili na rasilimali za pwani na baharini zinazozunguka visiwa vya Zanzibar.

Alisema sekta ya uvuvi ni muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar, hivyo serikali inafanya jitihada za dhati za kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, ili kuzalisha ajira kwa wananchi na kujipatia kipato kitakachowasaidia kuwakwamua dhidi ya umaskini.

"Mpango wa kununua vyombo umekamilika na tunaendelea kujipanga zaidi katika kutekeleza kuwapatia wavuvi vyombo vya kisasa na mitaji kwa ajili ya kuuza na kuimarisha hali zao," alisema.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya nane imejikita katika kuboresha masoko ya samaki yaliyopo na kujenga mapya, na kwamba suala hilo litakwenda sambamba na ujenzi wa kiwanda cha kuchakaza minofu na kusindika samaki kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya Zanzibar.

Akitaja vipaumbele ni sekta ya uvuvi mdogo mdogo na wa bahari kuu, ufugaji wa samaki, uchimbaji wa mafuta na gesi, utalii wa fukwe na michezo ya baharini.

Akiwasilisha mada ya dhana ya uchumi wa buluu, Ofisa Uratibu, Shaaban Hassan Ramadhan, alihimiza matumizi endelevu ya rasilimali za baharini, mito na maziwa kwa ajili ya ukuzaji uchumi, maendeleo ya kijamii na uhifadhi wa mazingira.

## Ismailia yajikita hifadhi mazingira

**Na Richard Makore,** MWANZA

JUMUIYA ya Ismailia nchini imeanzisha mpango maalum wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti pamoja na kutoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa jamii.

Mwakilishi wa Taasisi ya Aga Khan mkoani Mwanza, Mahaboob Ramji, alisema wameanza kwa kupanda miti 1,300 na kwamba wanaendelea na kazi hiyo kati ya miezi sita hadi mwaka mmoja.

Alisema Mwanzilishi wa Taasisi ya Aga Khan, alianzisha mpango huo ili kuisaidia jamii duniani, na kwamba kwa Tanzania walianza kazi hiyo juzi katika Mkoa wa Mwanza.

Alisema katika Soko la Kirumba mkoani Mwanza, wameanza kwa kuwasaidia mama lishe kwa kukarabati sehemu zao za kufanyia biashara.

Aliongeza kuwa katika ukarabati huo watajenga makabati maalum ya kuhifadhia vyombo vya mamalishe pamoja na kuwapatia meza na viti.

# Mgombea udiwani CCM apita bila kupingwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGOMBEA udiwani Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Victor Mmanywa, amepita bila ya kupingwa, baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutupilia mbali rufani ya Mgombea wa ACT-Wazalendo, Mvano Iddy, ya kupinga kutenguliwa katika uchaguzi huo.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa ACT-Wazalendo Jimbo la Shinyanga Mjini, Omari Gindu, alizungumza na Nipashe jana, alisema hawajaridhika na uamuzi ambao umetolewa na NEC, kumtoa mgombea wao kwenye kinyang'anyiro hicho.

Alisema kutokana na maamuzi hayo, hawana namna nyingine ya kufanya, baada ya wagombea tisa wa upinzani nao kuenguliwa.

"Tumeshapokea barua ya rufani ambayo tuliikata dhidi ya kupinga mgombea wetu wa kutenguliwa kugombea udiwani na tumeshawasiliana na Katibu Mkuu wa chama chetu... tumewaachia, lakini hatutashiliki shughuli zozote wala vikao vya kiserikali ambavyo vinashirikisha vyama vya upinzani," alisema Gindu.

Aidha wiki iliyopita msimamizi msaidizi wa uchaguzi Kata ya Ndembezi, Timothy Andrew, alimtangaza mgombea wa ACT-Wazalendo, Mvano Iddy na mgombea wa CCM Victor Mmanywa, kuwa ndiyo watagombea baada ya wagombea wengine tisa wa upinzani kuenguliwa kwa sababu ya kutokidhi vigezo, ikiwamo kutorudisha fomu.

Hata hivyo, baadaye msimamizi huyo msaidizi alitengua uteuzi wa mgombea wa ACT-Wazalendo, baada ya mgombea mwenzake wa CCM kuweka pingamizi kuwa hakujaza fomu ya maadili. Msimamizi huyo alisema baada ya NEC kufuatilia ilibaini ungufu huo na kuamua kumtengua.

Uchaguzi huo mdogo Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, ulipangwa kufanyika kufuatia kifo cha aliyekuwa diwani wa kata hiyo, David Nkulila Agosti mwaka huu. Pia alikuwa Meya wa Manispaa hiyo.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mtwara, Lucas Judah, akiweka wakfu jiwe la msingi katika ujenzi wa kanisa jipya la KKKT Dayosisi ya Masasi kwenye ibada maalumu iliyofanyika jana mjini Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# NHIF yaweka mikakati kukabili vikwazo afya

**Na Maulid Mmbaga**

KATIKA jitihada za kuwezesha vituo kuimarisha huduma za afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanzisha fursa ya mikopo ya vifaa tiba, ukarabati wa majengo na dawa ambazo zimesaidia kuleta mapinduzi makubwa ya huduma za afya nchini.

Hayo yalisema jana mkoani Dodoma na Mkurugenzi wa Utamaduni na Rasilimali Watu, Charles Lengeju, wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 20 ya utendaji kazi wa mfuko huo, ambapo alieleza kuwa awali huduma hizo hazikupatikana nchini na wagonjwa walilazimika kwenda nje ya nchi kupata matibabu.

Alisema miongoni mwa uimarishaji uliofanya na mfuko huo kwa udhamini wa serikali ni ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa na kufunga vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa.

Alisema hospitali hiyo imekuwa na msaada mkubwa wa huduma za kibingwa kwa wananchi wa ndani na nje ya nchi, ikiwamo upandikizaji wa figo.

Pia alisema hospitali zingine za rufani nchini kama KCMC, Mbeya, Bugando, na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) zimenufaika kwa kuimarisha miundombinu ya huduma na ufungaji wa vifaa tiba vya kisasa, ambavyo zimewezesha uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na tiba zake.

"Hadi kufikia Machi mwaka huu, zaidi ya vituo vya afya 316 nchini vimenufaika na mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 28.2. Pia mfuko umewapa wananchi wengi uhakika wa kupata huduma ya matibabu wakati wowote wanapopatwa na maradhi," alisema Lengeju.

Aliongeza kuwa mfuko pia umeboresha huduma kwa wanachama kwa kupanua huduma zitolewazo kwenye kitita cha mafao ambapo kwa sasa huduma nyingi zikiwamo matibabu ya Moyo, kusafisha figo na vipimo vikubwa vinalipiwa.

Aidha, mfuko umejipanga kutoa huduma bora kwa wanachama wake pamoja na kuhakikisha mifumo ya kihuduma katika vituo vya kutolea huduma inaboreshwa zaidi ili kila mwanachama aridhike na huduma anazopewa.

Aliwaomba wadau kuendelea kushirikiana na mfuko katika kutoa ushauri na mapendekezo ya namna bora ya kuboresha huduma zake.

Alieleza kuwa katika kurahisisha upatikanaji wa huduma, asilimia kubwa ya shughuli za mfuko huo zinafanyika kupitia TEHAMA, ikiwamo kumhakiki mwanachama kabla ya kupata huduma, ambapo alidai kuwa mfumo huo unasaidia kudhibiti udangajifu unaoweza kufanywa na baadhi ya wanachama na watoa huduma wasio waaminifu.

Alisema kwa kipindi cha miaka 20 ya utoaji huduma kwa wanachama wake moja ya jitihada ambazo mfuko umekuwa ukifanya ni kupanua wigo wa utoaji wa huduma bora na kuongeza usajili wa vituo katika ngazi mbalimbali ili kuweza kuwafikia wananchi kwa urahisi.

"Vituo vya kutolea huduma viliongezeka kutoka 3,197 kwa mwaka 2001 wakati mfuko unaanzishwa, na hadi kufikia Juni 2020 mfuko ulisajili jumla ya vituo 8,970 Tanzania Bara na Visiwani, pia nitoe wito kwa wananchi kujiwekea utamaduni wa kuwa na bima ya afya kwani itampa uhakika wa matibabu pindi anapopatwa na maradhi ya dharura," alisema Lengeju.

# TADB yakopesha mil. 436/- ujenzi kiwanda korosho

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeidhinisha mkopo wa Shilingi 435,500,000, kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda kidogo cha kusindika korosho, ili kuliongezea thamani zao sambamba na kuongeza pato la taifa pamoja na kuinua pato la mkulima.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa mradi wa ubunifu katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho chini ya Taasisi ya Care Tanzania, wilayani Mkinga, mkoni Tanga, Meneja wa Kanda ya Mashariki wa TADB, Jeremiah Jeremiah Mhada, alisema kuwa benki hiyo imeidhinisha mkopo huo ambapo zitatumika katika ujenzi wa kiwanda na ununuzi wa mashine na vifaa mbalimbali za kuendesha kiwanda hicho.

"Fedha hizo zitatoka kwa awamu, ikiwa ni kujenga miundombinu ya kiwanda na awamu ya pili kufadhili wakulima wa korosho, pembejeo zitakazowawezesha kuzalisha korosho kwa tija na kupata bei nzuri sokoni," alisema Mhada

Alieleza kuwa fedha zilizotolewa zitakwenda kusaidia katika kutengeneza ajira kupitia kazi ya ujenzi wa majengo ya kiwanda, pia kukiwezesha kiwanda mtaji wa kununua korosho kutoka kwa wakulima wadogo wadogo.

"TADB imetoa mkopo huu kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la korosho hali, itakayopelekea kuongezeka kwa mapato ya wakulima wa korosho, wilayani Mkinga, alisema Mhada na kuongezea kuwa kiwanda hicho kitaongeza thamani ya zao na kuhamasisha wakulima kufanya kilimo cha korosho kutokana na uhakika wa soko.

Mhada alisisitiza kuwa majukumu ya TADB ni kuhakikisha mageuzi yanafanyika katika sekta ya kilimo na kuwabadilisha wakulima kutoka kilimo cha mazoea na kufanya kilimo biashara na kuwafanya waweze kupita hatua kiuchumi kupitia shughuli za kilimo na kuwaunganisha na masoko kupitia chama cha msingi cha ushirika cha DUGA. Alieleza kwa sasa mafuta ghafi ya korosho yanauzwa katika Soko la Umoja wa Ulaya, Marekani, Japan na Korea, ambapo wasambazaji wakuu ni India na Brazil. Hivyo tukiweza kuzalisha wenyewe mafuta haya Tanzania itakuwa miongoni mwa wasambazaji wakuu wa bidhaa hiyo, Duniani.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha DUGA, Said Hassan Tuwano, aliishukuru benki ya TADB, pamoja na wawekezaji walioamua kuwekeza katika wilaya yao na kusema hii imeonyesha dhamira ya dhati ya kusaidia wakulima wadogo nchini.

"Nashukuru zaidi kwa kutupa asilimia 45 ya hisa kwenye kiwanda, hivyo zaidi ya wakulima 200 tutakuwa sehemu ya kiwanda na tumejipanga kuhakikisha tunaongeza idadi ya wakulima mpaka kufikia 2,500 katika wilaya yetu, ili tunufaike wote," alisema Tuwano.

Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Kanali Maulid Surumbu, aliwataka wadau wote kutekeleza majukumu yao kuhakikisha uzalishaji wa zao la korosho unaongezeka pamoja na kuhakikisha kiwanda kinakamilika, ili uzalishaji uanze msimu ujao wa mavuno.

Nipashe
TESA
Jumanne Septemba 28, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

## Kilimo, ufugaji shuleni, wazazi kuchangishana jeshi jipya la kupiga vita udumavu mkoa wa Pwani



Ukurasa 12

Elimu 'kivitendo' ni kichocheo kwa wanafunzi kupenda shule



Ukurasa 13

Kilimo ikolojia kinavyokomboa wanawake wakulima maskini

ELIMU
**NA GWAMAKA ALIPIPI**

UDHIBITI DAWA ZA KULEVYA

# Wigo ni mpana zaidi wamo madereva, wakala misitu, wanafunzi na majeshi

DAWA za kulevya zimewatumbukiza wengi kwenye mauti, magonjwa sugu, ulemavu na kuharibu mwelekeo wa maisha ya maelfu ya waraibu.

Wanapojitumbukiza kwenye biashara ya dawa hizo wanapuuza athari wakifikiria kupata pesa na buruduni zaidi, matokeo yake ni madhara na nguvu kazi hasa vijana kuwa hatarini kuangamizwa.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imeliona hilo na sasa inashirikiana na asasi za kiraia (AZAKI) kuelimisha umma athari za matumizi na madhara ya dawa hizo. Ripoti ya hali ya dawa za kulevya ya mwaka 2020 iliyotolewa na DCEA, inaeleza kuwa katika mwaka huo AZAKI 26 zimeelimiaha jamii athari za dawa hizo.

Elimu hiyo iliyolenga makundi mbalimbali ilitolewa kwenye vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, tovuti za taasisi, machapisho, maadhimisho ya kitaifa, sanaa na wasanii, klabu za kupinga dawa za kulevya, semina na makongamano.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe Kamishna wa Kinga na Tiba wa DCEA, Dk. Peter Mfisi, anaeleza kuwa mwaka 2020, ulifanyika uelimishaji kwenye sekondari na vyuo katika mikoa mbalimbali kwa kutumia.

Aidha, anasema ulifanyika uelimishaji kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika Kanda ya Ziwa, Kusini, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini.

Anaongeza kuwa ili kufanikisha operesheni za pamoja kutokomeza kilimo cha bangi na mirungi kwenye misitu, DCEA ilifanya uelimishaji kwa watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS). Uelimishaji ulifanyika maeneo ya mipaka ya Tunduma, Kasumulu, Namanga, Tarakea, Holili, Manyovu, Mabamba na Mtambaswala.

Anazungumzia kitisho cha bangi akisema: "Takribani watu milioni 269 duniani wenye kati ya miaka 15 hadi 64 walitumia dawa za kulevya mwaka 2018. Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumika zaidi duniani, mwaka 2018 watu milioni 192 waliivuta," anasema Dk. Mfisi.

Aidha, anasema mamlaka ilifanya uelimishaji kwa umma kwenye maadhimisho ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, kwamba ulifanywa na redio, machapisho, sanaa na wasanii, runinga, mitandao ya kijamii na tovuti ya mamlaka.

Anabainisha kuwa elimu pia ilitolewa katika maadhimisho ya kitaifa ya Nanenane Mkoa wa Simiyu pamoja na maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani mkoani Kilimanjaro.

Mbali na hilo, anasema mamlaka ilitoa elimu juu ya masuala ya udhibiti wa kemikali bashirifu kwa wadau 920 wakiwamo madereva wa malori ya kubeba kemikali 187, wasimamizi wa shughuli zinazohusu kemikali na wakaguzi 109, wajasiriamali wanaotumia kemikali 520.



Nguvukazi ikijimaliza kwa kujichoma dawa za kulevya. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, maofisa biashara 71 na maofisa wa serikali 33 na kwamba uelimishaji huo ulifanyika katika vituo mbalimbali vya forodha.

"Kemikali bashirifu hutumika kutengeneza dawa za kawaida za binadamu. Lakini, dawa hizo zikichepushwa zinaweza kutengeneza dawa za kulevya."

Anasema zina matumizi halali na ambayo siyo halali na baadhi ya mifano ya kemikali hizo ni pamoja na dawa kama methanol, clecio arthetic Acid, hydrochloric acid, sulphuric acid hizi ni dawa ambazo zina matumizi mbalimbali.

### UELIMISHWAJI NA AZAKI

Dk. Mfisi anabainisha kuwa wadau mbalimbali hushiriki katika kutoa elimu ya dawa za kulevya ili kuhakikisha jamii kubwa zaidi inafikiwa na elimu hiyo.

Baadhi ya asasi hizo ni Blue Cross Tanzania kutoka Arusha, YOVARIBE ya Dodoma, MEFADA kutoka Pwani, OYARB, Gift of Hope Foundation zote za mkoani Tanga, nyingine ni DAFCO ya Mwanza, Kihumbe, SETA, Changamoto ni matumani, Harakati Network Organization, Kibao Salama Foundation za mkoani Mbeya.

### CHANGAMOTO ZA KUDHIBITI

Kamishna wa Kinga na Tiba wa DCEA anasema zipo changamoto lukuki za kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini, lakini anataja kuu nane.

Mosi, anasema ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa Bahari ya Hindi husababisha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa mgumu.

Pili, anabainisha ni kubadilika mara kwa mara kwa teknolojia inayotumika katika biashara za dawa za kulevya, aidha uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya na nne ni unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za hizo kurudisha nyuma jitihada za matibabu.

Anagusia kukosekana kwa maabara ya uchunguzi ili kutafiti na kubaini dawa mpya za kulevya ni changamoto , lakini kuibuka kwa dawa mpya za kulevya (NPS) ambazo hazipo katika sheria za udhibiti wa kimataifa kunaongeza ukubwa wa tatizo.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA ANAELI MBISE

# Elimu ‘kivitendo’ ni kichocheo kwa wanafunzi kupenda shule



Watoto wakijifunza kuogelea, wanapofunzwa kwa vitendo ndivyo wanavyokuwa na uwezo zaidi wa kuelewa. **NA MPIGAPICHA WETU**

“SISI tunapenda na tunavutiwa na kujifunza kwa sababu ya kuona vitu tunavyofundishwa darasani. Tukiambiwa huyu ni simba, tunaiona na kuigusa sanamu yake.

Kuona na kugusa tunachofundishwa kunatusaidia kujua kwa wepesi mambo yanayohusu jamii zetu na yaliyomo nje ya upeo wetu.”

Ni ushuhuda wa mwanafunzi Kourtney Kibona wa shule ya msingi na awali ya Jubilation iliyoko Bunju Dar es Salaam, akizungumza na Nipashe.

Joeivan Kataraia ni Mwalimu Mkuu wa Jubilation, anayeyatolea ufafanuzi maelezo hayo akisema elimu ya kufundisha kwa matendo ni nyenzo ya ufundishaji kimafanikio kwa vile kila anachofunzwa mwanafunzi anakigusa na kukiona.

Wanafunzi wanafundisha kwa kutumia mbinu ya Maria Montessori, ikimaanisha wanafunzwa kwa matendo zaidi ili kurahisisha uelewa wa haraka kwa kile anachofunzwa darasani, anaongeza.

Anasema mbinu ya Montessori, ina faida kwa sababu wanafunzi wanapofundishwa nadharia wanapata fursa ya kuifanyia vitendo zaidi.

“Madarasa matatu yanatumika kwa ajili ya elimu ya awali na ndani ya darasa moja kati ya hayo ndipo tunawafundisha Montessori kwa kutoa vitu kwenye nadharia na kuviingiza kwenye matendo zaidi kwa kutumia vile anavyoviona kwa kuigusa kwa mfano mwanafunzi anafundishwa kuwa hii ni tufe, lakini anaiona,” anasema Kataraia.

> Katika kutekeleza hilo ndani ya shule tumefunga kamera za kurekodi matukio mbalimbali ‘CCTV’ kwenye kila eneo na hii inasaidia kama tatizo likitokea inakuwa rahisi kulifuatilia na kujua kiini chake.

“Elimu ya awali ni muhimu kwa sababu inamwezesha mwanafunzi kujua kusoma, kuhesabu na kuandika ndiyo maana shuleni hapa tunatumia maumbo tofauti baada ya nadharia kuwafundishia wanafunzi na imefanikisha waelewe kwa urahisi mno,” anaongeza.

Pamoja na utalaamu wa Montessori matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imewawezesha kufundisha kwa kutumia mtandao.

Kufundishia mtandaoni ni pamoja na kutumia runinga, ‘projector’, ‘power point’ ambavyo ni njia mbadala ya kutumia ubao na hii ni kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea dunia, anasema Kataraia.

### KUANDAA VIPAJI

Anazungumzia shule inavyoandaa wanafunzi wenye vipaji kama vya kuogelea, wacheza kandanda, mpira wa pete pamoja na wanamuziki.

“Kwa kutumia utaalamu wa Montessori tunagundua na kuibua vipaji tofauti vya wanafunzi wetu,” anasema Kataraia.

Anatoa mfano wa kutumia mikono kupanga tufe na vifaa vingine, yote yanaashiria kuna uhandisi unaochipuka ndani yake, anaongeza.

Anasisitiza upatinakaji wa miundombinu bora na ya kuridhisha imefanya ufundishaji na ujifunzaji uwe wa kuvutia kwa wanafunzi pamoja na walimu kutokana na uongozi wa shule kuwekeza kwenye eneo hilo.

Anasema ulinzi wa maisha ya watoto ni jambo muhimu na kuongeza kuwa wakati mwingine wanaweza kudhuriwa au kushambuliwa na kuwataka wadau kuweka uzio au kamera kulinda watoto.

“Katika kutekeleza hilo ndani ya shule tumefunga kamera za kurekodi matukio mbalimbali ‘CCTV’ kwenye kila eneo na hii inasaidia kama tatizo likitokea inakuwa rahisi kulifuatilia na kujua kiini chake. Kwahiyo ulinzi unaondoa mashaka kwa wazazi na walezi juu ya ulinzi kwa mtoto,” anasema Kataraia.

Mchungaji Emmanuel Sitta ni Ofisa Ustawi wa Jamii na Mshauri wa Jubilation akiwapa ushauri wa kisaikolojia kwa wanafunzi, walimu pamoja na wafanyakazi wengine kwa lengo la kuboresha na kufanya mazingira rafiki ya usomaji na ufundishaji.

“Shule inahusika kukuza wanafunzi kimwili, kisaikolojia, kiakili, kiuelewa na ufahamu wao kwa hiyo mshauri wao nahakikisha walimu na wanafunzi wanakuwa na munganiko,” anasema Sitta.

“Yaani mwalimu asidhani kazi yake ni kufundisha tu hapana atengeneze urafiki ambao unaokubalika, tunawajenga watoto kuishi kijamii pamoja na kuangalia utambuzi wao ili wasipotoke kimaadili,” anasisitiza.

Mwanasaikolojia huyo anasema wanawekeza zaidi kwa wanafunzi kimalezi ili yawe bora ili kupata wataalamu bora baadaye, ili wawe madakatari, wanasiasa, wahandisi na walimu pia.

Anazungumzia upembuzi wa kujua vipaji mbalimbali vya watoto na kuanza kuvikuza kwa ajili ya maisha bora ya baadaye.

Pamoja na umuhimu wa miundombinu iliyo bora ndani ya shule hiyo, mshauri huyo anaona pia uwepo wa muunganiko wa mafiga matatu kati ya walimu, wanafunzi na wazazi au wazazi ndiyo uliosaidia kuwajenga wanafunzi kuelewa vyema taaluma ya elimu inayotolewa.

Katika suala la kumudu masomo kwa wanafunzi Mchungaji Sitta anatoa wito na ushauri kwa jamii ya Shule ya Jubilation wakiwemo pia wazazi kuhakikisha kuna ufuatiliaji wa karibu kwa mwanafunzi atakayeonekana hamudu vyema masomo.

“Jambo jingine la kuzingatia kwa mtoto ni kujua uwezo wa kusoma, urafiki wa kijamii, utunzaji wa hisia, kukuza haiba ambazo zinapatikana kwa urahisi na mzazi. Hapa ndipo, hitaji huja kuelewa mtoto anafikiria nini, anafanyaje na ni mambo gani ambayo husababisha mabadiliko katika tabia ya mtoto,” anasema.

Hata hivyo, Mchungaji Sitta anasema mbinu ya wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani ni kwa kuwajengea uwezo wa kuandaa majaribio ya mitihani na hivyo kuondoa kabisa hofu juu ya kufanya vizuri katika masomo yao.

## Wigo ni mpana zaidi wamo madereva, wakala misitu, wanafunzi na majeshi

**INATOKA UK.11**

Anataja kuongezeka kwa matumizi na usafirishaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya ketamine, tramadol na tapentadol duniani kuwa ni tatizo.

Aidha, waraibu kukosa shughuli za kufanya wakati wakipata huduma za methadone na kukosekana nyumba za upataji nafuu na wakimaliza muda wao.

### HATUA ZA BAADAYE

Dk. Mfisi anabainisha kuwa hatua za baadaye kwanza ni kuimarisha sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya (sura ya 95) kwa kuhuisha mara kwa mara kulingana na mabadiliko.

Pili, anasema kupanua huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya, kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa hizo ndani na nje ya nchi na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali katika juhudi za kudhibiti.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Kilimo ikolojia kinavyokomboa wanawake wakulima maskini

## • Mbegu na pembejeo asili, mavuno tele

WAKATI gharama za mbegu na pembejeo za kilimo kama mbolea na viuatilifu zikipanda kwa kasi, udongo haujabaki salama umejaa tindikali (asidi) baada ya kuzidiwa na sumu za mbolea za viwandani, yote haya huongeza gharama za uzalishaji na mavuno haba.

Uzalishaji unapungua kwa sababu si wakulima wote wenye fedha za kununua mbolea za kisasa, mbegu na dawa za kuangamiza wadudu.

Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe ni moja ya maeneo yenye changamoto hiyo iliyowaathiri zaidi wanawake wakulima wadogo, kwasababu si wengi wanaomudu kununua mbegu na pembejeo za kilimo kutoka viwandani.

Ili kuwanusuru, Shirika la ActionAid na MIICO kupitia udhamini wa Shirika la Maendeleo la Uswiss (SDC) wamefunzwa utaalamu wa kujinasua na changamoto hizo kupitia mradi wa kilimo ikolojia.

Kinamama wanaunda majukwaa ya wanawake yanayojikita kwenye kilimo hicho kinachotunza mazingira, kutumia mbegu, pembejeo za asili zenye gharama ndogo.

Mradi wa kilimo ikolojia unadhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC) linaloshirikiana na ActionAid Tanzania na MIICO, anasema Meneja wa Taifa wa Mradi wa SDC, Samwely Mkwatwa.

Anasema unatekelezwa katika mkoani Mbozi katika kata tano za Zelezeta, Idiwili, Iyula, Hasamba na Itaka.

Anawaambia wanahabari waliotembelea mradi huo katika kata tano na kukutana na kinamama na wadau wanaozungumzia mafanikio ya mradi huo.

Anasema lengo ni kuboresha lishe ya familia, kukabiliana na udumavu na kuinua uchumi wa wakulima wadogo hawa wanawake kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inazalisha vyakula vingi lakini kuna changamoto ya udumavu.

Mradi unashirikisha wadau, maofisa ugani kwenye kata hizo na wanawake wakulima wadogo takribani 150 kutoka kata hizo tano wamefunzwa na wanalima kiikolojia na wameendelea kuwahamasisha wenzao, anasema Mkwatwa.

Licha ya Mbozi kuzalisha vyakula vingi, kinamama wameachwa nyuma kiuchumi, hawana fedha za kununua pembejeo lakini mila na desturi zinawabagua, hivyo ni njia mojawapo ya kuwainua kiuchumi na kuboresha maisha, anasema.



Cecilia Mwasembo, akielezea matumizi ya majani ya matwitwi kwa ajili ya kuzalishia mbolea. **NA MPIGAPICHA WETU**

### KILIMO IKOLOJIA NI NINI?

Ofisa Ugani na Mifugo wa Kijiji cha Itaka wilayani Mbozi, anayeshirikiana na jukwaa la kata hiyo, Elibariki Kiganga, anasema ni kilimo kinachozingatia hali halisi ya eneo bila kuathiri uasilia wa sehemu kinapofanyika.

"Kinatumia mbolea, mbegu na viuatilifu vya asili ili kulinda rutuba ya udongo, kupunguza gharama za uzalishaji na kulinda usalama wa chakula dhidi ya sumu zinazotumiwa kuhifadhi mazao".

"Ni kilimo kinachokabiliana au kudhibiti mabadiliko ya tabianchi ambayo pia husababishwa na matumizi makubwa ya pembejeo za viwandani, lakini ni nafuu kwa vile hakitumii gharama kubwa."

Anataja miti iitwayo 'matwitwi' kuwa inatumiwa kutengeneza mbolea ya asili, pia mboji na samadi zinatumika kupandia.

Anasema matwitwi yanapowekwa kwenye mimea ni sawa na mbolea ya 'nitrojen', ambayo inawezesha mimea kuzalisha chakula chake na kuwa na rangi ya kijani na inapokosekana inakuwa ya njano na haikui.

"Kina mama hao wanaotumia mimea ya asili iitwayo 'utupa' kuhifadhi nafaka na kudhibiti wadudu waharibifu kama pekecha."

### MBINU WANAZOFUNZWA

Cecilia Mwasembo ni Katibu wa Jukwaa la Wanawake la Kata ya Itaka, ni mkulima wa ikolojia na mtaalamu wa kuzalisha mboleo ya asili, anaelezea mchakato wake.

"Unajaza majani ya matwitwi kwenye jaba la ndoo mbili na nusu. Unakatakata vipande vya matwitwi na kuviloweka kwa siku 14. Unafunika na kila siku unayakoroga. Mbolea inakuwa tayari baada ya siku 14. Ni lazima kuchanganya kila siku." Anasema.

Ikishakuwa tayari urojo huo, unatumika kwa kipimo cha kikombe kimoja kukuzia kila mche wa mhindi wakati nusu kikombe hutumiwa kwenye mche wa mboga mfano bamia au ngongwe.

Anasema mbolea za asili za mboji na samadi hupandia wakati ya matwitwi hukuzia na huwekwa mara mbili na kwa mujibu wa Kiganga huongeza naitrojeni kwenye mimea.

Cecilia anazungumzia uzalishaji wa dawa ya kuhifadhia mazao ya 'utupa' akisema, "tunauchuma, kuutwanga, kuchanganya na maji na kuloweka saa12. Baada ya hapo tunanyunyuzia kwenye mazao na kuyaanika."

Anasema inaweza kutengenezwa jioni na kuanza kutumiwa asubuhi haina kemikali wala athari kwa binadamu.

"Mkojo wa ng'ombe na pilipili kichaa hutumiwa kuua wadudu wanaoshambulia mboga shambani. Lita ya mkoo inahifadhiwa juma zima kisha huchanganywa la lita 5 za maji ni dawa ya kuua wadudu kwenye mboga. Baada ya siku tatu zinachumwa na kuliwa ni salama," anasema.

### TIJA KILIMO IKOLOJIA

Rose Mwahalemi, ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wa Kijiji cha Iyula, kilichoko kata ya Iyula, anasema: "Kilimo ikolojia kimetuwezesha wanawake kulima hata kama hatuna fedha za kununua mbegu, mbolea na viuatilifu. Tunazalisha kwa sababu vitu vya asili havina gharama."

Wanawake kwenye majukwaa hayo wanasema awali walikuwa wanawaogopa maofisa ugani na walikuwa wakilima kienyeji lakini sasa wanawatumia na wanatafuta utaalamu wakiwa na changamoto.

"Kwa ujumla kinamama tumebadilika tumekuwa ni sehemu ya uzalishaji. Mwaka jana nililima kilimo cha gharama nilitumia karibu Shilingi 470,000 kulima eka moja kununua mbegu, mbolea na dawa za viwandani. Nikavuna magunia sita. Lakini msimu huu nimetumia kilimo ikolojia nimepata magunia 21 na gharama imepungua hadi Shilingi 220,000," anasema Rose.

Baadhi ya maeneo wakulima wanatumia mbegu za chotara (hybrid) na kuna hisia kuwa mbegu za asili kama za mahindi na maharage zimetoweka. Inakuwaje wakulima wilayani Mbozi wawe na mbegu za asili?

Ofisa Kilimo wa Kata ya Iyula, Khalid Mchomvu, anasema mbegu hizo zipo, hazijatoweka na baadhi ya wakulima vijijini wanazo, lakini pia zinapatikana kwenye vituo vya taasisi za utafiti wa kilimo ndiyo maana kilimo hicho kinawezekana.

Anasema licha ya mbegu hizo kukomaa kwa muda mrefu na wakati mwingine mvua zinaweza kuwa haba na kuwashauri wamwagilie mazao.

### KIMEELIMISHA WANAWAKE

Kinamama wanaolima kilimo hicho wanaeeleza kuwa kimewaelimisha kwa kuwakutanisha na wataalamu kwa vile zamani waliwaogopa maofisa ugani.

"Tulikuwa tunalima kienyeji leo hii nilazima kuwasiliana ofisa ugani pia nao wanatutembelea na tunawatafuta siyo kama zamani," anasema Esta Angomwisye wa Jukwaa la Iyula.

Anaungwa mkono na Alinikisa Mbeye wa Jukwaa la Kata ya Zelezeta, anayesema kwa kuwatumia maofisa ugani anatumia mbolea za kisasa kwa ufanisi zaidi.

"Zamani nilikuwa naweka bila utaratibu, leo nafuata maelekezo na utaalamu wa maofisa ugani kwa mfano nafamu nikilima kwa pembeo za viwandani napanda na DAP, kuanzia Desemba mvua zikianza. inayofuata ni UREA au NPK ni ya kukuzia naweka mahindi yenye majani matano mpaka sita na kukuzia awamu ya pili ni wakati kuna majani nane mpaka 1O" anasema.

Kinamama hawa wanakumbushia kuwa kabla ya ujio wa mradi huo, walikuwa hawawezi kuwasiliana na ofisa ugani wakiwaogopa na kuhisi kuwa walikuwa 'mabosi'wa serikali.

"Wanawake hatukuzungumza nao labda mume wako awasiliane naye, apewe maelekezo naye akijulishe hasa wale wenye ndoa. Lakini leo tunapata elimu na mafunzo bila kikwazo iwe kwenye jukwaa au mkulima binafsi. Tunafahamu mambo mengi kuliko zamani hatuna vikwazo," anasema Rose Mgalla wa Kata ya Hasamba.

"Tunashukuru ActionAid na MIICO kutuondolea vikwazo hivi vya huduma za ugani zilizotutesa kwa miaka mingi," anasema Rose anayezalisha mahindi na kahawa.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Kilimo, ufugaji shuleni, kupiga vita udumavu mkoa wa Pwani



Wanafunzi wa Shule ya Bokotimiza, uongozi wa shule pamoja na viongozi wa serikali wakinywa uji kuhamasisha kuwapo chakula shuleni. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

MKOA wa Pwani unahimiza kuwapa wanafunzi chakula shuleni katika jitihada za kupunguza udumavu wa kiasi kikubwa unaoshuhudiwa katika eneo hilo lenye vyakula vya kila namna pamoja na samaki kutoka Bahari ya Hindi.

Udumavu unatokana na utapiamlo ambao ni ukosefu wa lishe bora tatizo linalochangia mtoto kuwa na umbile na kimo kisichoendana na umri wake.

Mtoto akiwa na udumavu hata maisha ya kawaida mitaani yanakuwa magumu kwake, usikivu darasani unakuwa mdogo matokeo yake ni ufaulu duni kwenye masomo, mitihani na maisha.

Licha ya maendeleo na juhudi za serikali katika kutatua tatizo la lishe duni, utapiamlo upo na unasumbua licha ya kuwapo jitihada na ahadi za kupunguza tatizo hilo kwa watoto chini ya miaka mitano.

Mkoa wa Pwani ni kati ya maeneo yenye udumavu kwa watoto takwimu zikionyesha kuwa una asilimia 23.8 ya watoto wenye udumavu wakati wastani kitaifa ni asilimia 30.1.

Tathmini inayofanyika kila baada ya miezi sita kufuatia mikataba ya lishe waliyosaini wakuu wa mikoa na wilaya kwenye uhamasishaji wa lishe umekuwa ukiendelea katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

> “Tafsiri yake ni kuwa katika watoto 100 wenye umri chini ya miaka mitano 24 wamedumaa na hata wakiwa watu wazima itakuwa ngumu kuinua uchumi wa familia na taifa.

Uhamasishaji huo unafanyika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya huko, wazazi na wanawake wajawazito wanapewa elimu ya vyakula wanavyotakiwa kula kipindi chote.

Upo mkataba wa lishe waliosaini wakuu wa mikoa na TAMISEMI unaolenga kusimamia masuala ya lishe bora kupunguza athari za utapiamlo katika mikoa na taifa.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge, anatoa maelekezo kwa viongozi kuhakikisha chakula kinapatikana shuleni kukabiliana na udumavu.

“Tafsiri yake ni kuwa katika watoto 100 wenye umri chini ya miaka mitano 24 wamedumaa na hata wakiwa watu wazima itakuwa ngumu kuinua uchumi wa familia na taifa,” anasema Kunenge.

Anawaagiza viongozi wa halmashauri na waratibu wa afya kitengo cha lishe kuhakikisha chakula kinapatikana shuleni.

Kunenge anatoa maelekezo hayo katika kikao kazi cha tathmini ya mkataba wa lishe katika mkoa huo kilichofanyika mjini Kibaha na kuwashirikisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi na viongozi wa halmashauri.

Anasema lishe bora katika jamii ni kichocheo cha maendeleo endelevu katika nyanja mbalimbali hususan ya viwanda, afya, kilimo, elimu, biashara na uchumi lakini hayo yatafikiwa endapo athari za lishe duni zitadhibitiwa.

Kunenge anaongeza kuwa katika kila darasa lenye watoto 45 kati yao 11 wanaweza kuwa wadumavu na hawafundishiki na kusisitiza upatikanaji wa chakula shuleni.

“Upatikanaji huu unaweza kufanyika kwa shule kuzalisha matunda, mboga, mihogo, mahindi na mpunga pia ufugaji wa kuku, bata na sungura kulingana na hali halisi ya maeneo ya shule,” anasisitiza.

Anasema endapo utekelezaji huo utafanyika wanafunzi watakuwa na afya bora na kuelewa wanayofundishwa.

Ofisa lishe Mkoa wa Pwani Pamela Meena, anasema wanakabiliwa na kikwazo cha uhaba wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii waliojengewa uwezo katika masuala ya lishe na usimamizi usioridhisha wa mkataba wa lishe ngazi ya kata na vijiji;

Maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani yameanza kutekelezeka kwa Kata ya Tumbi, Kibaha kutokana na uhamasishwaji unaofanywa na Diwani wa Tumbi Raymond Chokala.

Wazazi wa wanafunzi wa Shule ya Boko Timiza Kata ya Tumbi wameridhia kuchangishana fedha kwa ajili ya chakula kwa watoto walioko shuleni.

Katika kikao kilichofanyika hivi karibuni kikitishwa na Diwani Chokala wamekubaliana kila mzazi kuchangia Sh. 200 kwa siku ili watoto wapate chakula, kufuatia maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge.

Akizungumza baada ya kikao hicho Chokala anasema atafanya vikao na wazazi kwenye shule za msingi tano zilizopo katika kata hiyo kushauriana kwa pamoja namna ya wanafunzi kupata chakula.

Anasema kuwapo kwa chakula shuleni kutapunguza udumavu, lakini ni njia kuinua ufaulu kwa wanafunzi wa kata hiyo.

Anaongeza: Nimeanza na shule ya Boko Timiza hii imekuwa na ufaulu hafifu mambo mengi yanaelezwa kuchangia hilo ikiwamo la mwamko mdogo wa wazazi katika elimu, lakini kikao changu cha leo kimekuwa na mafanikio makubwa kwangu na nimetoa sufuria ili wanafunzi waanze kupikiwa,” anasema.

Anaeleza kuwa mwitikio unaoonyeshwa na wazazi hao unatoa mwanga wa mabadiliko kuanzia kwenye ufaulu wa mitihani lakini wazazi kushiriki moja kwa moja kuwafuatilia wanafunzi.

Anasema sasa wanafunzi wa shule hiyo wataanza kupata chakula lakini wamekubaliana waanze kilimo cha viazi lishe kuongeza chakula shuleni.

Diwani huyo anaahidi kuendelea na vikao kwenye shule nyingine zilizosalia kuzungumza na walimu na wazazi kuweka utaratibu wa kupatikana kwa chakula shuleni.

Lishe bora inaweza kuokoa maisha ya watu million 3.7 ifikapo mwaka 2025 kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na shirika hilo Septemba mwaka 2019 huduma za afya zinapaswa kujikita zaidi katika kuhakikisha kila mtu anapata lishe bora.



# Rukwa yaondolewa adha kusafiri kwa baiskeli, punda

**Na Grace Mwakalinga,**
SUMBAWANGA

WANANCHI wa Kata za Muze na Kalumbaleza mkoani Rukwa wanatarajia kuondokana na kero ya muda mrefu ya kutumia umbali wa saa zaidi ya 12 kwa usafiri wa baiskeli na punda kwenda mikoa ya Tabora na Katavi, baada ya Wakala wa Barabara (TANROADS) kuanza ujenzi wa daraja ambalo litakuwa kiunganishi kwa maeneo hayo.

Kwa mujibu wa TANROADS Mkoa wa Rukwa, Mhandisi, Mgeni Mwanga, alisema Sh. bilioni 2.5 zitatumika kukamilisha ujenzi wa daraja la Kalumbaleza ambalo litakuwa kiunganishwa kwa wakazi wanaosafiri kwenda mikoa ya Tabora na Katavi.

Mhandisi Mwanga amesema hadi sasa ujenzi wa daraja hilo umekamilika kwa asilimia 85 na kwamba hadi kufikia Oktoba 14, mwaka huu ujenzi utakamilika.

Alisema mkataba wa ujenzi wa daraja hilo ulisainiwa Januari, lakini kutokana na mvua nyingi, walilazimika kuanza ujenzi Juni, na kwamba mkandarasi wa mradi huo ni Kampuni ya Sumri Entreprises wa mkoani Rukwa.

"Gharama ya awali ilikadiriwa katika mradi huo ilikuwa ni Sh. bilioni moja, lakini kutokana na uharibu wa mvua zilizonyesha kipindi cha masika gharama za ujenzi ziliongezeka na kufikia Sh. bilioni 2.5 kutokana na kazi za nyongeza kama vile urefu wa daraja kutoka mita 2.5 hadi mita 5.1, midomo kutoka mitatu hadi 10 pamoja na mabega sehemu zote nne ya daraja," alisema Mhandisi Mwanga.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alielezwa kufarijika na kasi ya ujenzi wa daraja hilo, na kwamba fedha hizo zimetolewa kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuondokana na adha ya usafiri kutokana na miundombinu ya barabara na daraja kutokuwa rafiki.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa maradaja kwenye maeneo mbalimbali mkoani humo na kwamba hadi sasa ujenzi wa madaraja matatu unaendelea katika kata hizo. Aidha, aliwashauri wananchi kuacha kufanya shughuli za kilimo na uendelezaji wa makazi karibu na vyanzo vya maji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi sambamba na kukwamisha wa miundombinu ya barabara pamoja na madaraja.

Baadhi ya wananchi wa maeneo hayo wameishukuru serikali kuwajengea daraja la Kalumbaleza kwa maelezo kuwa kwa sasa wataweza kusafiri mikoa ya Tabora na Katavi bila tatizo. Dickson Kisalala, alisema ujenzi wa daraja hilo umewawezesha vijana kupata ajira na kinamama kufanya shughuli za mama lishe pamoja na usombeleaji wa mawe na mchanga.

Meneja wa Mradi wa daraja hilo kutoka Kampuni ya Sumri, Said Rajabu, alisema moja ya vikwazo walivyokabaliana navyo ni mvua nyingi za masika ambazo zilichelewesha ujenzi huo ambao ungetakiwa kuanza mwezi Januari.



Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Kusini (Njombe), Isaya Mengele, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jana, kuhusu hatima ya mgogoro unaofukuta kuhusu kuihamisha Dayosisi ya Konde kutoka Mjini Tukuyu kwenda Halmashauri ya Jiji la Mbeya, ambapo amesema uamuzi huo wameubariki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Lami kuunganisha Mbeya, Tabora, Singida

**Na Grace Mwakalinga,**
CHUNYA

SERIKALI imepanga kujenga kilomita 58 za barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na mikoa ya Tabora na Singida kuanzia katika Mji wa Makongolosi wilayani Chunya kwa kiwango cha lami katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Hayo yalisemwa juzi na Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alipokuwa anazungumza na wananchi wa Mji wa Makongolosi kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo.

Alisema kwa sasa ujenzi wa barabara ya Chunya - Makongolosi yenye urefu wa kilomita 39 umekamilika, hivyo katika bajeti iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni zimetengwa fedha kwa ajili ya kuendeleza barabara hiyo na kwamba barabara hiyo itakuwa inajengwa kwa awamu tofauti.

Alisema mbali na barabara hiyo, pia zipo barabara ambazo zitaboreshwa na serikali ili kuwasaidia wananchi wa maeneo ya pembezoni mwa miji kusafiri na kusafirisha mazao yao bila vikwazo vya aina yoyote.

"Serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya uboreshaji wa barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika wilaya yetu, hivyo naamini kuwa barabara nyingi zitaboreshwa," alisema Kasaka.

Vilevile alisema katika wilaya hiyo kuna vijiji 12 na vitongoji 14 ambavyo havijafikiwa na umeme, lakini akadai kuwa tayari makandarasi wanaendelea na kazi ya kusambaza nishati hiyo kwenye vijiji vyote.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha vijiji vyote nchini vinaunganishiwa nishati hiyo ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao, ikiwamo uanzishwaji wa viwanda vidogo.

## Wadau wawapiga jeki wanahabari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKURUGENZI wa Shule za Paradise mikoa ya Mbeya na Dar es Saalam, Ndele Mwaselela, amewaahidi kuwanunulia gari waandishi wa habari wa Mbeya kwa ajili ya kufanyia shughuli zao za kihabari.

Mwaselela alitoa ahadi hiyo wakati wa hafla ya chakula cha pamoja cha usiku kilichowahusisha wanahabari, wabunge na baadhi ya wadau ambapo alitumia nafasi hiyo kuwaambia waandishi wa habari mambo mbambali ya kujikwamua kiuchumi.

Alisema gari hilo atawakabidhi wanahabari Julai mwakani kwa utaratibu maalum, huku akiwasisitiza kuunda umoja imara ambao utawawezesha kupata fursa mbalimbali ili kujiingizia kipato.

"Nimewaita wanahabari kwa lengo la kujadili masuala muhimu ya ninyi kujikwamua kiuchumi mmekuwa na jitihada za kuwasemea wenzenu kuwasaidia kusonga mbele ili hali maisha yenu ni magumu ni wakati sasa mshikamane ili msonge mbele," alisema Mwaselela.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, aliwaahidi wanahabari kupatia Sh. milioni moja kwa ajili ya kutunisha mfuko wao kwa kujikwamua na uchumi, huku milioni mbili kwa ajili ya ununuzi wa gari ambalo aliahidi Mwaselela kununua.

Alisema wanahabari ni daraja kati ya wadau, serikali na wananchi na kwamba wamesaidia kwa kiasi kikubwa kubadilisha maisha ya watu.

Aliahidi kuongeza ushirikiano kwa wanahabari na kwamba atahakikisha Mbeya inakuwa na umoja na kusonga mbele kimaendeleo.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema aliwaahidi wanahabari kuwapatia karasha la madini ya dhahabu kwa maelekezo kuwa watalitumia kwa ajili ya kujiingizia kipato.

Sambamba na hilo, alichangia shilingi milioni mbili kwa ajili ya ununuzi wa gari la wanahabari pamoja na milioni moja kwa a
jili ya kutunisha mfuko wa wanatasnia.

Mmoja wa wanahabari, Martha Sambo, aliwashukuru wadau hao kwa kuamua kuwainua kiuchumi na kwamba ni fursa kwao kubadilisha maisha kutoka hatua moja kwenda nyingine.

**Aliahidi kuongeza ushirikiano kwa wanahabari na kwamba atahakikisha Mbeya inakuwa na umoja na kusonga mbele kimaendeleo.**





# Ahamasisha wananchi kujitokeza kupiga kura

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, amewataka wananchi wa Jimbo la Konde kujitokeza kupiga kura katika uchaguzi mdogo wa jimbo hilo unaotarajiwa kufanyika Oktoba 9, mwaka huu.

Aliwataka wananchi wa jimbo hilo wasiwe na uoga wowote wajitokeze kwa wingi na kumchagua mgombea wa ACT-Wazalendo, Muhammed Said Issa, ili awawakilishe katika Bunge kwa ajili ya kupaza sauti zao.

Jussa aliyaeleza hayo jana huko Msuka katika kiwanja cha Okapi, Wilaya ya Micheweni Pemba wakati wa uzinduzi wa kampeni za mgombea wa chama hicho katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde.

"Tumchagueni Muhammed ili awe sauti ya watu wa Konde na Wazanzibari kwa ujumla akasimamie maslahi yetu na vizazi vyetu," alisema Jussa.

Aliwataka wanachama wa chama hicho Jimbo la Konde wasiwe tayari kulaghaiwa au kurubuniwa na vyama vingine vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi huo.

"Chama pekee kinachoweza kuleta maendeleo ni ACT- Wazalendo viongozi wake wanauthubutu wa kudai chochote chenye maslahi ya Zanzibar," alisema.

"Tulikuwa tukimsikia mbunge wetu ambaye ni marehemu alivyokuwa akiitetea Zanzibar Marehemu Khatib Said, kwa hiyo tumchagueni Muhammed ili akaendeleze pale alipopaacha marehemu."

Aliwataka vijana wasiwe wenye kukata tamaa katika kutafuta mabadiliko ya Zanzibar kutokana na vitimbi vinavyofanywa na baadhi watu aliowataja kuwa hawaitakii mema Zanzibar.

Alisema uchaguzi uliopita mgombea aliyejiuzuru, Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na kile alichodai watu ambao hawana nia njema na Zanzibar waliingilia uchaguzi na kuuvuruga.

Kaimu Katibu Mkuu ambaye ni Katibu wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Salim Biman, aliwataka wananchi wa Konde waende kwenye vituo vya kupigia kura kwa kujiamini kuwa mgombea wao atashinda na atatangazwa na yeyote atakayehujumu uchaguzi chama kitapambana naye na kuwahakikishia kuwa haki itasimama.

Kwa upande wake mgombea wa jimbo hilo kupitia ACT-Wazalendo, Muhammed Said Issa, alisema yuko tayari kuwa mbunge wa watu wa Konde ili kuwasemea katika chombo cha kutunga sheria.

Mgombea huyo anagombea nafasi hiyo kwa mara ya pili baada ya uchaguzi mdogo wa awali mshindi kutoka CCM Shekha Mpemba, kujiengua katika nafasi hiyo kabla ya kuapishwa.




Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT -Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, akimtambulisha kwa wapigakura mgombea wa chama hicho katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kondo nafasi ya ubunge, Muhammed Said Issa, katika uzinduzi wa kampeni uliofanyika Viwanja vya Okapi Msuka Wilaya ya Micheweni Jimbo la Konde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waandishi habari waelezwa njia ya kutatua migogoro

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANDISHI wa Habari, Asasi za Kiraia na Watendaji wa Serikali wametakiwa kuwa wabunifu na kutumia njia sahihi katika utatuzi wa migogoro ndani ya jamii.

Hayo yalielezwa na Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa Jenga Amani Yetu, Khamis Haroun Hamad, wakati akifungua mkutano wa majadiliano baina ya Watendaji wa Serikali, Asasi za Kiraia pamoja na waandishi wa habari juzi mjini hapa.

Aliwataka washiriki hao kuwa na ushirikiano wa pamoja katika kufuatilia na kutatua migogoro inayoikabili jamii inayowazunguka.

Alisema kuwa waandishi wa habari, wana asasi za kiraia pamoja na watendaji wa serikali wana jukumu kubwa la utatuzi wa migogoro katika jamii inayowazunguka hivyo wanapaswa kuwa wabunifu na kutumia njia zilizosahihi ili wasiwe chanjo cha kuendeleza migogoro.

Alisema, jambo la msingi ni kuwa waangalifu wakati wa utatuzi wa migogoro na kuielewa vyema jamii ambayo wanafanyia kazi.

"Mnapaswa kuwa na ushirikiano wa pamoja wakati wa ufanyaji kazi wenu, lakini pia jambo la msingi ni kuwa waangalifu wakati wa utatuzi ili kila upande uweze kufaidika," alisema.

Alisema, katika utendaji kazi wao wa kila siku wanapaswa kuzingatia namna ya kulinda amani ya nchi.

Naye Mratibu wa Mradi wa Jenga Amani yetu Zanzibar, Jamila Maoud, aliwataka washiriki wa mkutano huo kuwa na busara na hekima wakati wa utatuzi wa migogoro inayoikabili jamii ili muwafaka upatikane.

"Unapotumia weledi, hekima na busara wakati wa utatuzi wa migogoro huwa ni nyenzo kubwa inayosaidia kwa kiasi kikubwa kutatua migogoro kwa njia ya amani," alisisitiza.

Washiriki wa mkutano huo walisema kuwa jamii inakabiliwa na migogoro mingi ikiwamo ya ardhi na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mradi wa Jenga unatekelezwa na Shirika la Search for Common Ground pamoja na kituo cha huduma za sheria Zanzibar na wafadhili wakuu wa mradi huo ni Umoja wa Ulaya.

# Serikali yataka wazee kuchanja chanjo ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya na Ustawi wa Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazruwi, amewataka wazee kuchanja chanjo ya corona ili kujikinga na athari zinazoweza kujitokeza.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wazee Jimbo la Mtoni.

Alisema maradhi hayo yanawaathiri zaidi wagonjwa na wazee na lengo la kuwapatiwa chanjo hiyo kutawasaidia kupunguza nguvu za maradhi.

Aidha, alisema matibabu yake ni gharama kubwa hivyo hakuna budi kupatiwa chanzo hizo ili kuwaepushia wakati yatakapowapata.

Alisema serikali imejipanga kuwapatia chanjo hizo wazee popote walipo katika maeneo yao bila usumbufu na kuwaomba wananchi kuunga mkono juhudi hizo ili ziweze kufanikiwa.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni, Hussein Ibrahim Makungu, alisema wanachukua juhudi mbalimbali za kuboresha maisha ya wazee hao, lakini baadhi yao wanakabiliwa na tatizo la kukosa matunzo ya uhakika.

Aliwaomba viongozi wa majimbo kuandaa mikakati madhubuti ya kuwasaidia wazee katika maeneo yao kwa sababu wametoa mchango mkubwa kwa familia na taifa kwa ujumla.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA IPO MWANANYAMALA KWA KOPA. INA VYUMBA VITATU VYA KULALA, SEBULE, JIKO, CHOO NDANI NA NJE. INA UMEME, MAJI NA FENCE. KWA MAWASILIANO PIGA: 0754409991.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAYA ALI JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye index namba S.2417/0033 Kilichotolewa na **HAKI SEKONDARI - TANGA** mwaka 2016. Cheti cha kidato cha nne Chenye index namba **P.1553-0013** kilichotolewa na **PONDENI SEKONDARI - PEMBA** mwaka **2017.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya **Polisi CHK/RB/2458/2021.**

116479802

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRAIDEN MKARUMANYIKA JAFES** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3262-0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BURUNGURA SEKONDARI mwaka 2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/460696/2021.**

116479902

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI MRATHI NA. 104 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MUSIMU MUKAMA KAYUMBA MWOMBAJI**
**DONALD BWIRE MASATU**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki na Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 21 Mwezi wa 10, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo **tarehe 24 Mwezi wa 9, 2021.**

116479202

FORM No.A/1

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIAJUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF MOMBA**
**AT CHAPWA**
**CIVIL CASE NO. 6 OF 2021**
**ISMAIL FADHIL MBAGA………………………………..PLAINTIFF (S)**
**VERSUS**
**KELVIN FIULD……………………DEFENDANT (S)**

**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.v.r 1Civil Procedure Code)**

**To: KELVIN FIULD**
**WHEREAS** the above named Plaintiff(s)hase/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in dublicacte within twenty one (21) days of service of this notice upon you.if ther is more than one Plaintiff,additional copies of your written statement of defence must be filed suffiecient on each of the plaintiffs.If thre are more defendants than one and the defence is not joint defence,thre must be filed suffiecient copies for service on each of the other defendants.
**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing of the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.
**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also hase been fixed for order befor Hon T.A LYON-SRM Judge/Magistrate on the **20 day of 10,2021 at 07:30 O'clock** in forenoon/afternoon.

**GIVEN UNDER MY HAND THE SEAL OF THE COURT**
**This 21 day of 09 ,2021**
T.A.LYON
REGISTRAR/MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
MOMBA

116479502

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO. 67 OF 2021**
**SAMEER MOHAMED…………………PLAINTIFF**
**VERSUS**
**THE TEMEKE MUNICIPAL COUNCIL & OTHERS……………DEFENDANTS**
**TO: (1) SOPHIA BAKARI IMONJE, (2) JACKSON BARIKIEL ULOTU, (3) SAMI GEORGE MAHENGE, (4) WAKUBEMBA BAKARI BUSOLO, (5) BAKARI ATHUMAN NDOLWA.**

**WHEREAS:** The above named **PLAINTIFF** has institute the **PLANT** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 11th day of O**CTOBER 2021 at 09:00AM Before Hon. A. MSAFIRI, JUDGE**, in the morning to answer the said APPEAL and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your **REPLAY.**
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court, this **7th day of SEPTEMBER, 2021.**

DEPUTY REGISTRAR

116480002

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 109 OF 2021**
**In the matter of the Estate of the late ALEX MADUHU BUGOMOLA of Mipango Miyuji ward within City Council of Dodoma**
**AND**
**In the matter of Application for letter of Administration by FAUSTINE ALEX BUGOMOLA**
**GENERAL CITATION**
***(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)***

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 September,2021.
Dated at Dodoma this 28 day of **SEPTEMBER 2021.**
Presented for filling this **14 day of 09 2021.**

116480202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GIDU SHABANI MSITU**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG.** yenye namba ya usajili **MC 501 ACC** yenye Chassis no. **LBRSPJB58E9037105**
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya jeshi la polisi.
**KAH/RB/1648/2021.**

116477502

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

116480202

# Sudan yaishutumu Ethiopia kuvuruga usalama wake

**Khartoum, SUDAN**

SUDAN imesema imezuia jaribio la Jeshi la Ethiopia, kuingia kwenye ardhi yake, kwenye mpaka wa Al-Fashaqa karibu na mpaka wenye mzozo wa Tigray.

Mkuu wa Jeshi la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, amethibitisha jaribio hilo na kusema, inaonyesha ni namna gani jeshi la nchi hiyo linailinda nchi, dhidi ya jaribio la mapinduzi ya kijeshi, kama ilivyoshuhudiwa wiki iliyopita.

Hata hivyo, Jeshi la Ethiopia halijazungumzia ripoti za Sudan, ingawa ofisa wa serikali aliliambia Shirika la Aljazeera kwamba, wanajeshi wa nchi hiyo, hajawavuka mpaka kuingia katika nchi hiyo jirani.

Mwaka jana serikali ya Khartoum, ilituma wanajeshi wake katika mpaka wa Al-Fashaqa, wakati uongozi wa Ethiopia ulipotuma wanajeshi katika Jimbo la Tigray, kupambana na waasi.

Mapigano katika Jimbo la Tigra, yamesababisha maafa makubwa ya watu, huku wengine wakikimbilia katika nchi jirani ya Sudan.

Uhusiano kati ya Ethiopia na Sudan, umeendelea kuwa mbaya kufuatia hatua ya Addis Ababa kuendelea na mradi wa kutumia maji ya Mto Nile, kujaza bwawa lake la kuzalisha umeme.

**RFI**

# Dunia ina hifadhi silaha za nyuklia 14,000

**New York, MAREKANI**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) António Guterres, amesema dunia imeendelea kuwa tishio kwa takribani miongo minne kutokana na kuhifadhiwa kwa silaha za nyuklia licha ya kwamba ni marufuku.

Guterres aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya kimataifa ya kukomesha silaha za nyuklia.

Alisema, wito kwa nchi zote zinazoshikilia teknolojia ya nyuklia kutia saini mkataba wa kina wa kupiga marufuku matumizi ya nyuklia (CTBT), ambao ulipitishwa mwaka 1996 na umesainiwa na nchi 185.

Alisema, ili mkataba wa CTBT uanze kutumika, lazima utiwe saini na kuridhiwa na nchi 44 zilizo na teknolojia ya nyuklia, ambazo nane bado hazijaridhia mkataba huo, China, Misri, India, Iran, Israel, Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Korea , Pakistan na Marekani. Tumebaki katika hali hii ya sintofahamu kwa muda mrefu," alisema Katibu Mkuu.

Aliongeza ni wakati wa kuondoa silaha za nyuklia na kuanzisha enzi mpya ya mazungumzo, uaminifu na amani, na kuabainisha kushughulikia tishio la silaha za nyuklia.

"Imekuwa msingi wa kazi ya Umoja wa Mataifa tangu kuanzishwa kwake, lilipopitishwa azimio la kwanza la Baraza Kuu kuhusu silaha hizo mwaka 1946, likitaka kuondolewa silaha zote za atomiki na silaha zingine zote zinazoweza kusababisha maangamizi makuu kote duniani."

Alisema kwamba, ingawa idadi ya silaha za nyuklia zimekuwa zikipungua kwa miongo kadhaa, zingine 14,000 zimehifadhiwa kote duniani na kuifanya dunia kukabiliwa na hatari kubwa zaidi ya nyuklia kwa karibu miongo minne.

"Nchi zinaendelea kuimarisha vituo vya silaha za nyuklia, na tunaona ishara zenye kutia wasiwasi za mashindano mapya ya silaha. Ubinadamu bado unaendelea kuwa karibu na silaha za maangamizi ya nyuklia, suala ambalo halikubaliki."

**UN**



Mgombea wa Chama cha Kisoshalisti chenye mrengo wa kati-kushoto (SPD), kiti cha ukansela Olaf Scholz akizungumza jana, jijini Berlin, nchini Ujerumani baada ya kushinda kiti hicho, kwenye uchaguzi wa wabunge na kansela, uliofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: AP**

# Msoshalisti mwenye mrengo wa kati ashinda Ujerumani

**Berlin, UJERUMANI**

CHAMA cha siasa cha Kisoshalisti chenye mrengo wa kati-kushoto (SPD), kimepata ushindi mwembamba kukiangusha Chama cha Muungano wa Kihafidhina wa CDU-CSU, ambao umekuwa ukiongozwa na Kansela Angela Merkel anayemaliza muda wake.

Matokeo ya awali ya uchaguzi uliofanyika siku ya Jumapili, yanaonyesha, chama cha SPD kimepata ushindi mwembamba wa asilimia 25.7 na kukishinda chama cha CDU, ambacho kimeibuka katika nafasi ya pili kwa asilimia 24.1.

Chama cha SPD kiliongoza kwa asilimia mbili zaidi, wakati huu matokeo ya mwisho yakisubiriwa.

Kiongozi wa chama cha SPD Olaf Scholz amejitokeza na kusema, matokeo yanaonyesha chama chake kimeshinda na kupewa nafasi ya kuongoza nchi hiyo ya Bara la Ulaya.

Armin Laschet, kiongozi wa chama cha CDU licha ya kuwa nyuma, ana imani kuwa atafanikiwa kuunda serikali na kumrithi Kansela Merkel, ambaye uongozi wake wa miaka 16, unafika mwisho.

Hii ndio mara ya kwanza baada ya muda mrefu chama cha CDU kupata matokeo mabaya.

Kufuatia vyama vya SDP na CDU-CSU, kuonyesha nia ya kuunda serikali kutokana na uchaguzi wenye ushindani mkali, upande wowote unaweza kufanya hivyo, iwapo utapata washirika wanaohitajika kuunda serikali ya muungano.

Iwapo hali itakuwa hivyo, Kansela Merkel ataendelea kuongoza hadi pale serikali ya muungano itakapoundwa labda kufikia baadaye mwezi Desemba.

**RFI**

# Taliban yapiga marufuku kunyoa ndevu

**Kabul, AFGHANISTAN**

TALIBAN imepiga marufuku, vinyozi katika Mkoa wa Helmand, kutowanyoa au kuwapunguza ndevu wanaume, wakisema hatua hiyo inakiuka sheria ya Kiislamu.

"Mtu yeyote anayekiuka sheria hiyo, ataadhibiwa," Askari wa Taliban wamesema.

Baadhi ya vinyozi katika Mji wa Kabul walisema, kwamba pia wao walipata maagizo kama hayo.

Maagizo hayo yalieleza kuhusu kurudishwa kwa sheria kali kama zile zilizokuwapo wakati kundi hilo lilipokuwa madarakani awali, licha ya ahadi ya kwamba litaanzisha serikali itakayokuwa na misimamo ya wastani.

Tangu ilipochukua madaraka mwezi uliopita, Taliban imewapatia adhabu kali wapinzani wake.

Siku ya Jumamosi , wapiganaji wa kundi hilo, waliwapiga risasi na kuwaua watekaji wanne na miili yao kuzungunshwa katika barabara ya Mkoa wa Herat.

Katika ilani iliyochapishwa katika saluni, Kusini mwa Mkoa wa Helmand, maofisa wa Taliban walionya vinyozi, lazima wafuate sheria ya Kiislamu katika kunyoa nywele za kichwani na ndevu.

"Wapiganaji hao wanaendelea kuja na kutuagiza kutonyoa ndevu." alisema kinyozi mmoja mjini Kabul'.

Mmoja wao aliniambia kwamba wanaweza kutuma maofisa kuchunguza, ili kutukamata."

Walimtaka kutofuata mitindo ya Marekani na kutowanyoa watu ndevu zao.

Wakati wa uongozi wa kwanza wa Taliban kuanzia mwaka 1996 hadi 2001, kundi hilo lilipiga marufuku mitindo tofauti ya nywele na kusisitiza wanaume wafuge ndevu.

Tangu wakati huo, unyoaji wa ndevu na nywele fupi miongoni mwa wanaume Waafghan umekuwa maarufu.

Baadhi ya vinyozi, ambao hawakutajwa majina, ili kuwalinda, walisema sheria hizo mpya zinawapa mazingira magumu ya kujipatia kipato.

"Kwa miaka mingi saluni yangu ilikuwa ikivutia vijana wadogo wanaotaka kunyolewa wanavyotaka, ili kuonekana vijana wa kisasa. Hakuna haja ya kuendelea na biashara hii," kinyozi mmoja aliambia BBC.

**BBC**

**"Wapiganaji hao wanaendelea kuja na kutuagiza kutonyoa ndevu" alisema kinyozi mmoja mjini Kabul'.**

# NYOTA WATATU YANGA KUIKOSA KAGERA SUGAR

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga mapema tu jana kimewasili salama mjini Bukoba tayari kwa mchezo wao wa kesho dhidi ya Kagera Sugar, lakini kitawakosa nyota wake watatu Saido Ntibazonkiza, Dickson Ambundo na Yassin Mustafa ambao ni majeruhi.

Yanga itashuka katika Uwanja wa Kaitaba kesho kuvaana na wenyeji Kagera Sugar kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu Bara baada ya msimu mpya kuanza rasmi juzi.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akizungumzia mchezo huo, alisema baada ya kufika salama Bukoba wanaendelea na maandalizi ya mwisho ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya na kufanya vizuri kwenye ligi hiyo.

Alisema ana imani ligi ya msimu huu itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zimejiandaa vizuri kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tuko fiti na tayari kwa mchezo huo, nina matarajio hautakuwa rahisi kwa sababu Kagera Sugar watahitaji kutumia vema uwanja wa nyumbani kwa kutafuta matokeo chanya," alisema Nabi.

Kuhusu Ntibazonkiza, Mustafa na Ambundo, Nabi alisema atawakosa nyota hao kwa kuwa bado hawajawa fiti baada ya kupona majeraha yao, lakini tayari wameanza mazoezi mepesi kabla ya kurejea uwanjani moja kwa moja.

Aidha, Nabi alisema ujio wa Cedric Kaze katika benchi lake la ufundi, ni faraja kwake kwa sababu amewahi kuifundisha timu hiyo, na uelewa wake mzuri wa soka la Tanzania kutamrahisishia kazi.

Kwa upande wa Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema sherehe za ubingwa wa Ngao ya Jamii zimekwisha na sasa wanaenda kuanza ligi na matarajio yao ni kupata alama tatu dhidi ya Kagera Sugar.

"Sasa tunaenda kuanza Ligi Kuu, na kila mechi kwetu ni fainali, tutamheshimu kila mpinzani tutakayekutana naye, kikubwa wanachama tudumishe umoja na ushirikiano ili kufikia malengo yetu ya ubingwa wa Ligi Kuu," alisema Manara.

Wakati Yanga wakisema hayo, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, alisema anatambua ukubwa wa Yanga na wanawaheshimu, lakini kamwe hawaogopi.

Alisema ana kikosi chake kipo imara na tayari kwa ajili ya kuingia katika mapambano ya kupata pointi muhimu kwenye ligi hiyo.

"Ninaendelea kutoa maelekezo kuhakikisha wachezaji wote wanakuwa fiti na kutengeneza kombinesheni na uelewano uwanjani kabla ya kukutana na Yanga," alisema.

**MSHINDI...**




Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Martini Ngoga (kulia), akimkabidhi zawadi mbalimbali mshindi wa jumla wa mashindano ya 'Diplomatic Golf', Dier Mohamed, yaliyofanyika kwa siku mbili Septemba 25 na 26, mwaka huu, katika viwanja vya Kilimanjaro Gofu (Kiligolf) vilivyoko jijini Arusha, pia Wizara ya Maliasili na Utalii ilizindua zao jipya la Utalii wa Gofu. **MPIGAPICHA WETU**

# TPLB na matarajio ya Ligi Kuu bora zaidi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imeanza jana, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), imesema inatarajia kuwa na msimu bora zaidi kwa msimu huu kuliko uliopita.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, amesema kauli mbiu yao ni kwamba kila msimu uwe bora kuliko uliopita, hivyo ana matarajio makubwa ubora kuongezeka msimu huu hasa kutokana na vitu vyote vilivyofanyika, ikiwamo udhamini na kufuatwa kwa taratibu zote na kanuni, wahudhuriaji viwanjani na watazamaji, watarajie kuona Ligi Kuu bora na yenye ushindani wa aina yake.

"Kila kitu kilichotakiwa kumefanyika, tunatarajia kuona msimu bora zaidi kwa sababu sisi kauli mbiu yetu ni kwamba kila msimu uwe ni bora kuliko uliopita," alisema Kasongo.

Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, Ligi Kuu Tanzania Bara inakwenda kuchezwa ikiwa na timu 16.

Mara ya mwisho ilikuwa ni msimu wa 2017/18, lakini baada ya hapo ndipo timu ziliongezeka msimu wa 2018/19 na kuwa 20, ambazo nazo zilikuwa zikipungua mbilimbili kila msimu.

Naye mchezaji wa zamani wa Pan African na Taifa Stars, ambaye amewahi kuwa kocha wa klabu mbalimbali, ikiwamo Prisons, Mohamed Richard 'Adolf', amesema Ligi Kuu msimu huu itakuwa bora kama viongozi wa klabu hawatoweka maslahi yao mbele.

Alisema kutokana na udhamini uliowekwa na Kampuni ya Azam Media Ltd, anatarajia kama pesa zikitumika kuzihudumia klabu, basi timu nyingi zitaimarika na kuwa na ligi bora.

"Lakini kama wakiweka maslahi yao mbele, pesa zitaliwa na wachezaji wataendelea kukabiliwa na ukata, basi hakuna ambacho kitakuwa kimeboreshwa kwenye ligi," alisema.

## Wasanii watakiwa kuunda jukwaa lao

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kinathamini na kutambua michango ya sanaa nchini, hivyo kitakwenda kutatua kero wanazokutana nazo ili waweze kufikia malengo yao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Katibu wa Itikati na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka katika jukwaa la wasanii lililoandaliwa na Kampuni ya Marketing Africa, ambapo alieleza chama chake kitaendelea kuweka misingi imara ya kuendeleza sanaa nchini kama walivyoahidi katika ilani yao.

Shaka aliwataka wasanii kuandaa jukwaa ambalo watakutana nao na watamwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasikiliza kwa pamoja na kuona namna gani ya kuwasaidia ili changamoto zao zitatuliwe.

Alisema wanadhamira njema ya kukuza na kuwathamini wasanii na Rais Samia ameanzisha Wizara Maalum ya Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa lengo la kushughulikia changamoto za wasanii zilizopigiwa kelele kwa muda mrefu.

## BMT yatimua viongozi TAVA

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limesimamisha viongozi wa Chama cha Mchezo wa Wavu Tanzania (TAVA), kutokana na kadhia iliyojitokeza kwa timu ya Taifa ya mchezo huo na kuondolewa katika mashindano nchini Rwanda.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana Kaimu Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha, alisema timu hiyo iliondolewa katika mashindano hayo yaliyofanyika Septemba 7 hadi 15, mwaka huu kwa uongozi kushindwa kulipa ada za mashindano na gharama za malazi ikiwamo hoteli waliyofikia.

Alisema BMT imefanyia uchunguzi suala hilo na kujiridhisha kwamba tukio la timu hiyo kufukuzwa nchini Rwanda na kutia aibu taifa ni uzembe wa viongozi wa chama hicho.

"Kabla ya timu hiyo kuondoka nchini, BMT tulikutana na viongozi wa TAVA kuongea nao na kujiridhisha kuhusu gharama na kwa upande wetu serikali tulitoa kiasia cha Sh. milioni 11.7 kwa gharama zote za ndege kwenda na wao kuahidi kwa maandishi kuwa gharama nyingine watapata mdhamini," alisema Msitha.

Alisema baada ya kukutana waliwashauri, uongozi wa TAVA kubaki nchini endapo watakosa uhakika wa wadhamini, lakini walilazimisha kusafiki kwenda nje ya nchi wakiwa hawana hela ya kulipa ada ya ushiriki.

"Kwa sababu hizo tumewaondoa viongozi wa TAVA na hawataruhusiwa kabisa kujihusisha na uendeshaji wa chama kuanzia sasa," alisema.









# RASHFORD KURUDI, KUIVAA LEICESTER

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amedokeza kwamba, Marcus Rashford anaweza kurejea dimbani baada ya kufanyiwa operesheni.

Nyota huyo anatarajiwa kurejea kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Leicester City, Oktoba 16, mwaka huu.

Mshambuliaji huyo alifanyiwa upasuaji wa bega wakati wa kipindi cha majira ya joto na bado hajahusika na mechi yoyote ya 'Mashetani Wekundu' hao kwa msimu huu wa 2021-22.

Hivi karibuni Rashford alipigwa picha akiwa kwenye mazoezi, na kulikuwa na madai kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa England angeweza kuwapo dimbani kabla ya mapumziko ya kimataifa.

Hata hivyo, Solskjaer aliiambia tovuti rasmi ya Manchester United kwamba, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kurejea baada ya seti nyingine ya mechi za kimataifa Oktoba.

'Mashetani Wekundu' wana mechi dhidi ya Villarreal na Everton kabla ya kusafiri kwenda Uwanja wa King Power Oktoba 16, mwaka huu kucheza dhidi ya Leicester.

Rashford, ambaye alikuwa na mchango mkubwa kwa nchi yake kwenye Euro 2020, licha ya shida zake za majeraha, alifunga mabao 21 na kutoa asisti 15 kwenye mechi 57 za Man United kwa msimu uliopita.

# Nasri astaafu kucheza soka

**PARIS, Ufaransa**

SAMIR Nasri amethibitisha kwamba amestaafu kucheza soka la ushindani katika umri wa miaka 34.

Mchezaji huyo wa zamani wa Ufaransa alitangaza uamuzi huo kupitia Canal+, Jumapili, ambako kwa sasa anafanya kazi ya uchambuzi wa soka kwenye kituo hicho.

Nasri aliibukia Marseille na akahamia Arsenal mwaka 2008, akitumia miaka mitatu kwenye dimba la Emirates kabla ya kujiunga na Manchester City.

Kule City, Nasri alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu England, taji la EFL na Ngao ya Jamii.

Alijiunga na Sevilla kwa mkopo msimu wa 2016-17 na alionekana kuimarika kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ingawa hakuwa na mkataba wa kudumu.



Pia alicheza kwa muda mfupi nchini Uturuki katika klabu ya Antalyaspor, lakini Nasri alikatisha mkataba wake Januari 2018, kabla ya kufungiwa miezi sita na Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA), kwa kuvunja sheria ya matumizi ya Dawa za Kuongeza Nguvu Michezoni (WADA), kosa alilolifanya Desemba mwaka 2016.

Kufungiwa huko ndiko kulikomfanya Nasri kutokuwa tena na mapenzi na soka, huku mchezaji huyo mara zote akisisitiza hakuwa na kosa.

"Nilihukumiwa kwa kosa ambalo sikulifanya na hilo lilibadilisha mahusiano yangu na soka," alisema kupitia Canal+.

Nasri alirudi kucheza kwa muda mfupi na West Ham msimu wa 2018-19, akicheza jumla ya mechi tano za Ligi Kuu England.

## HABARI MICHEZO

,737,060

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 02.10.21 | 17:00 | Derby vs Swansea | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 2. 02.10.21 | 17:00 | Peterborough vs Bristol City | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 3. 02.10.21 | 17:00 | Luton Town vs Huddersfield | 2.39 | 3.25 | 2.86 |
| 4. 02.10.21 | 17:00 | Hull City vs Middlesbrough | 2.86 | 3.25 | 2.39 |
| 5. 02.10.21 | 17:00 | Blackpool vs Blackburn | 2.86 | 3.16 | 2.45 |
| 6. 02.10.21 | 17:00 | Barnsley vs Millwall | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 7. 02.10.21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.40 | 3.47 | 2.78 |
| 8. 02.10.21 | 19:30 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.15 | 2.58 |
| 9. 02.10.21 | 22:00 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.14 | 3.32 | 3.47 |
| 10. 03.10.21 | 16:00 | Tottenham vs Aston Villa | 2.14 | 3.46 | 3.36 |
| 11. 03.10.21 | 16:00 | Crystal Palace vs Leicester | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 12. 03.10.21 | 18:00 | Lille vs Marseille | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 13. 03.10.21 | 18:30 | Liverpool vs Manchester City | 2.75 | 3.39 | 2.52 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 28 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 2061 | Skra Czestochowa vs Lech Poznan | 11.57 | 6.94 | 1.16 |
| 17:00 | 4472 | Dunarea Calarasi vs FC Politehnica Iasi | 4.07 | 3.63 | 1.74 |
| 19:00 | 4355 | KS Gornik Polkowice vs Gornik Leczna | 3.43 | 3.43 | 1.95 |
| 19:45 | 1855 | Shakhtar Donetsk vs Inter | 5.21 | 4.31 | 1.57 |
| 19:45 | 2923 | Ajax vs Besiktas | 1.13 | 8.22 | 18.04 |
| 20:29 | 4348 | Kszo Ssa Ostrowiec Sw. vs GKS Tychy | 3.96 | 3.82 | 1.72 |
| 20:30 | 3417 | VfR Garching vs SV Kirschanschoering | 3.25 | 3.73 | 1.93 |
| 21:45 | 1172 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.91 | 3.06 | 2.47 |
| 21:45 | 1236 | QPR vs Birmingham | 2.07 | 3.30 | 3.45 |
| 21:45 | 1324 | Rotherham vs AFC Wimbledon | 1.70 | 3.70 | 4.64 |
| 21:45 | 1388 | Bromley vs Grimsby | 2.63 | 3.31 | 2.48 |
| 21:45 | 1442 | St Ives Town vs Barwell | 2.18 | 3.75 | 3.00 |
| 21:45 | 1751 | Morecambe vs Lincoln | 3.02 | 3.27 | 2.29 |
| 21:45 | 1847 | Plymouth vs Crewe | 1.85 | 3.56 | 3.95 |
| 21:45 | 2108 | Cambridge Utd vs Gillingham | 2.45 | 3.21 | 2.82 |
| 21:45 | 2211 | Glenavon vs Larne | 2.90 | 3.75 | 2.22 |
| 21:45 | 2585 | Glentoran Belfast vs Linfield Belfast | 2.20 | 3.50 | 2.82 |
| 21:45 | 2675 | MK Dons vs Fleetwood Town | 1.83 | 3.55 | 4.04 |
| 21:45 | 3080 | Ballymena Utd vs Dungannon Swifts | 1.30 | 5.24 | 7.38 |
| 21:45 | 3445 | Folkestone Invicta vs AFC Hornchurch | 2.09 | 3.59 | 2.96 |
| 21:45 | 3499 | Merthyr Town vs Tiverton Town | 2.44 | 3.65 | 2.44 |
| 21:45 | 3668 | Huddersfield vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 21:45 | 3682 | Cardiff vs West Bromwich | 3.40 | 3.25 | 2.11 |
| 21:45 | 3934 | Banbury United vs Biggleswade Town | 1.58 | 4.16 | 4.54 |
| 21:45 | 3978 | Ipswich vs Doncaster | 1.76 | 3.60 | 4.34 |
| 21:45 | 4069 | Sunderland vs Cheltenham | 1.60 | 3.94 | 5.13 |
| 21:45 | 4196 | Woking vs Chesterfield | 3.52 | 3.52 | 1.94 |
| 21:45 | 4299 | Leiston vs Needham Market | 1.81 | 3.77 | 3.62 |
| 21:45 | 4374 | Wigan vs Sheffield Wed | 2.32 | 3.26 | 2.96 |
| 21:45 | 4431 | Charlton vs Bolton | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 21:45 | 4449 | Shrewsbury vs Wycombe | 3.21 | 3.26 | 2.19 |
| 21:45 | 4675 | Burton vs Portsmouth | 2.86 | 3.21 | 2.42 |
| 21:45 | 4882 | Taunton Town vs Yate Town | 1.63 | 3.88 | 4.46 |
| 21:45 | 4897 | Bowers Pitsea vs Corinthian Casuals | 1.89 | 3.63 | 3.44 |
| 21:45 | 5148 | Utd of Manchester vs Scarborough Athletic | 2.42 | 3.43 | 2.56 |
| 21:45 | 5254 | Preston vs Stoke City | 2.78 | 2.93 | 2.68 |
| 21:45 | 5335 | Hull City vs Blackpool | 2.44 | 3.06 | 2.96 |
| 21:45 | 5534 | South Shields vs Lancaster City | 1.76 | 3.73 | 3.88 |
| 21:45 | 5841 | Haringey Borough vs Potters Bar Town | 2.06 | 3.43 | 3.14 |
| 21:45 | 5872 | Bromsgrove Rovers vs Hednesford Town | 2.22 | 3.48 | 2.81 |
| 21:45 | 5911 | Oxford Utd vs Accrington | 1.79 | 3.70 | 4.04 |
| 22:00 | 1080 | Paris St Germain vs Manchester City | 2.91 | 3.50 | 2.32 |
| 22:00 | 1603 | Borussia Dortmund vs Sporting Lisbon | 1.34 | 5.42 | 7.62 |
| 22:00 | 2035 | Porto vs Liverpool | 4.50 | 3.95 | 1.71 |
| 22:00 | 4379 | Real Madrid vs Sheriff Tiraspol | 1.13 | 7.85 | 20.04 |
| 22:00 | 4432 | La Serena vs Everton Vina del Mar | 2.99 | 3.14 | 2.26 |
| 22:00 | 4544 | AC Milan vs Atletico Madrid | 2.87 | 3.17 | 2.52 |
| 22:00 | 5514 | Avai vs Londrina PR | 1.56 | 3.63 | 5.62 |
| 22:00 | 5953 | RB Leipzig vs Brugge | 1.48 | 4.70 | 5.80 |
| 23:00 | 3575 | Universitario Popayan vs Tigres FC (COL) | 1.82 | 3.25 | 4.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# GUARDIOLA AFUNGUKA SILVA KUONDOKA CITY




**MANCHESTER, England**

NYOTA wa Manchester City, Bernardo Silva, anaweza kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England, kwa mujibu wa Pep Guardiola.

Silva alihusishwa na mpango wa kuondoka City wakati wa kipindi cha dirisha la usajili la majira ya joto, huku Atletico Madrid na Barcelona wakihusishwa naye, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ureno alibakia hapo Manchester.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ameanza katika mechi tano kati ya sita za City kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku akifunga bao la ushindi wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Leicester City.

Baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye ushindi wa Jumamosi wa bao 1-0 dhidi ya bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Chelsea, Guardiola alimsifia Silva.

"Kitu pekee anachotaka Bernardo ni kuwa na furaha, hapa au sehemu nyingine.

"Ninachotaka ni furaha yake kwa sababu yeye ni mtu ambaye anastahili vitu bora zaidi," alisema Guardiola akinukuliwa na BBC Sport.

"Pia ni mchezaji anayevutia si jukumu lake kucheza kama kiungo mchezeshaji, lakini anajua namna gani anacheza."

Silva ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu England mara tatu tangu alipojiunga na City mwaka 2017.




# Dybala, Morata kuikosa Chelsea Uefa Jumatano

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri amethibitisha kwamba, Paulo Dybala na Alvaro Morata hawataichezea Juventus kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea baada ya kuumia dhidi ya Sampdoria.

Bianconeri hao walipata ushindi wa pili mfululizo kwenye Serie A, huku wote Dybala na Morata wakiumia na hivyo hawatakuwapo kesho, Jumatano kwenye mchezo wa Ulaya wa Kundi H dhidi ya mabingwa hao watetezi.

Dybala alifunga bao la ufunguzi wakati Juve wakijivuta hadi nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Serie A, wakipitwa pointi nane na vinara AC Milan.

Awali Allegri alionyesha kutokuwa na wasiwasi juu ya majeraha ya wachezaji hao, lakini sasa amethibitisha kwamba, watakuwa nje ya dimba.

"Tutaangalia namna ya kucheza dhidi ya Chelsea bila Dybala na Morata," alisema Allegri akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Kwa sababu si mchezo wa kuamua hatima. Mchezo muhimu zaidi wa kufuzu hatua inayofuata ni ule dhidi ya Zenit."

Michezo
Jumanne Septemba 28, 2021
Nipashe



Aubameyang awavulia kofia makinda
UKURASA 21

# SIMBA SC KUANZA KUTETEA UBINGWA

●●● Kamwaga aachia ngazi, huko Azam yashikwa, Mbeya Kwanza FC na Namungo zaanza ligi kwa ushindi huku...

**Adam Fungamwango na Tunu Hassan, TUDARCo**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, Jumamosi iliyopita, mabingwa watetezi, Simba leo wataanza kibarua cha kuutetea ubingwa wao, kwa kuwavaa Biashara United kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume, Musoma mkoani Mara.

Simba inayowania kutwaa ubingwa mara ya tano mfululizo itakuwa na kibarua kizito cha kurudisha imani kwa wanachama na mashabiki wake ambao wanaona timu yao imepungua nguvu msimu huu, tangu kuondoka kwa wachezaji Luis Miquissone na Clatous Chama ambao wamepigwa bei.

Hata hivyo, Simba inaingia kwenye uwanja huo ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kushinda mechi zote ilizocheza dhidi ya wenyeji wao kwenye Ligi Kuu.

Ikiwa ugenini, Uwanja wa Karume, Simba imeifunga Biashara United mara zote tatu ilizokutana nayo tangu ipande na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2018/19.

Aprili 27, 2019, ilishinda mabao 2-0, yote yakiwekwa wavuni na John Bocco msimu wa 2018/19, uliofuata ilishinda tena 2-0, yaliyofungwa na Meddie Kagere na Miraji Athumani, Septemba 29, 2019, huku msimu uliomalizika ikishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Bernard Morrison, Februari 18, mwaka huu.

Kati ya hao, wachezaji ambao wanaweza wakacheza ni Bocco na Kagere, kwani Morrison bado anatumikia adhabu ya kukosa mechi tatu, aliyoipata kwenye mechi ya Kombe la FA mjini Kigoma na Miraji akiwa ameshaondoka kwenye kikosi hicho na sasa yupo KMC FC.

Baada ya kichapo cha bao 1-0, makocha na viongozi wa Simba wamekuwa wagumu kuongea chochote, lakini wote wamekuja na kaulimbiu moja isemayo 'tutarudi tukiwa imara zaidi.'

Kwa upande wa Meneja wa Klabu ya Biashara United, Frank Wabare, amesema maandalizi yote yamekamilika na kwamba Uwanja wa Karume ni sehemu ambayo itakuwa ngumu kwa wageni wote watakaokanyaga.

"Wala siyo Simba tu, hapa Uwanja wa Karume patakuwa pagumu kwa wageni msimu huu, tunaanza na hao Simba," alisema Wabare.

**TUPO FITI...**



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. Timu hiyo itashuka Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume, Musoma leo kuvaana na wenyeji, Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara leo. **PICHA: SIMBA**

Wakati huo huo, Kaimu Ofisa Habari wa Simba Ezekiel Kamwaga, amemaliza rasmi kipindi chake cha miezi miwili akiwa anakaimu nafasi hiyo na Ijumaa iliyopita aliagwa rasmi. Kutokana na hatua hiyo, Simba sasa itamtangaza ofisa habari mpya ambaye atachukua mikoba hiyo ya Kamwaga, ambaye aliikaimu baada ya uongozi wa klabu hiyo kuridhia ombi la Hajji Manara la kuachia ngazi.

Kwingineko katika msimu mpya wa Ligi Kuu Bara ulioanza jana, Mbeya Kwanza FC ilianza vema baada ya kuwachapa wenyeji wao Mtibwa Sugar kwa bao 1-0 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Mabatini mkoani Pwani huku Azam FC ikilazimisha sare ya 1-1 ugenini Uwanja wa Mkwakwani, Tanga dhidi ya Coatal Union wakati Namungo FC yenyewe ikiutumia vema uwanja wa nyumbani kwa kushinda 2-0 dhidi ya Geita Gold FC.

## Mkude arejeshwa Stars kuivaa Benin

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Jonas Mkude, amerejeshwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, 'Taifa Stars' na kuwa miongoni mwa wachezaji 25 wa timu hiyo walioitwa kujiandaa kwa mchezo dhidi ya Benin kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Stars inatarajia kuingia kambini Oktoba 3, kujianda na mechi hiyo dhidi ya Benin itakayopigwa Oktoba 7, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kwenda kurudiana ugenini siku tatu baadaye.

Nyota huyo wa Simba hakuitwa kwa muda mrefu katika kikosi hicho cha Stars kutokana na kuwa nje akitumikia adhabu ya klabu yake hiyo, lakini sasa amejumuishwa baada kurejeshwa kikosini katika klabu yake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Stars, Kim Poulsen, alisema amemrejesha Mkude kwa sababu ya uwezo wake alionyesha kwenye mechi za kirafiki.

Alisema amewaacha nyota watatu wa Azam FC akiwamo Mudathiri Yahya, Ayoub Lyanga na Abubakar Salum, (Sure Boy) kutokana na sababu za kiufundi.

"Ninachagua wachezaji wa timu ya Taifa kutokana na ubora mchezaji alionyesha kwenye timu yake au unaonyesha anapokuwa timu ya Taifa. Nimemrejesha John Bocco ambaye alikuwa majeruhi," alisema Poulsen.

Wachezaji wengine walioitwa na kocha huyo ni Aishi Manula (Simba), Metacha Mnata (Polisi Tanzania), Ramadhan Kabwili (Yanga), Shomari Kapombe, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Erasto Nyoni na Kenedy Juma (Simba), Dickson Job na Bakari Nwamnyeto (Yanga), Lusajo Mwaikenda na Edward Manyama (Azam FC), Nickson Kibabaje (KMC) Meshack Mwamita (Gwambina FC), Novatus Dismas (Maccabi Tel Aviv-Israel).

Wengine ni Mzamiru na Bocco (Simba), Feisal Salum (Yanga), Iddy Seleman Musa na Abdul Hamis Seleman (Azam FC), Mbwana Samatta (Royal Antwerp-Ubelgiji), Reliants Lusajo (Namungo FC) na Simon Msuva (Wydad AC-Morocco).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >